# Nipashe

Jumatatu Julai 27, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580294

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

n digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



## Familia yaweka wazi sababu kifo cha Mkapa

UKURASA 2




UKURASA 11




Baadhi ya waombolezaji wakitoa heshima zao za mwisho mbele ya mwili wa Rais mstaafu, Benjamin Mkapa, katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Maelfu Dar wamuaga

• **Taasisi** zaguswa, siri ya kuzikwa kijijini Lupaso yaelezwa... *Endelea Uk. 2,4,7,8,18*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

Fursa kwa Wagombea! 2020




Gazeti la Nipashe linatoa fursa kwa wagombea wote wa vyama vya siasa kunadi sera zao kupitia kurasa zetu kwa gharama nafuu.

Wasiliana nasi
The Guardian Limited
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

## ...Alivyoliliwa kimataifa

UKURASA 3

**MICHEZO** MKAPA AMEZIBEBA SIMBA, YANGA UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Maelfu Dar wamuaga

**Na Elizabeth Zaya**

MAELFU ya wananchi jana walijitokeza katika uwanja wa Uhuru jiji ni Dar es Salaam, kuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa awamu ya Tatu, Benjamini Mkapa.

Jana ilikuwa siku ya kwanza kwa wananchi kuaga ikiwa ni kati ya siku tatu zilizotengwa kwa ajili ya kuaga mwili huo, huku Rais wa Tanzania, John Magufuli akiongoza waombolezaji hao.

Wengine waliojumuika ni Makamu wa Rais, Samia Hassan Suluhu, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi , Zanzibar, Seif Ali Idd na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Msafara huo ulianzia Hospitali ya Jeshi ya Lugalo majira ya saa 2:30 asubuhi, huku Helkopita ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), na Jeshi la Polisi nchini, zikiimarisha ulinzi angani,

Msafara huo ulipita katika barabara za Mwenge, Ali HAsasan Mwinyi, Morocco, Daraja la Salender, Ocean Road, Posta ya zamani, Kituo kikuu cha Polisi, mzunguko wa barabara ya Bandari, Barabara ya Kilwa na Uhasibu, ulifika viwanja vya Uhuru majra ya saa Uwanja 9:42 asubuhi.

Kando kando mwa barabara hizo wananchi walijitokeza na kumwaga maua barabarani.

Baadhi ya wakazi hao walioyokuwa na mabango yaliyokuwa na ujumbe mbalimbali, miongoni mwao yakiwa yameandikwa ujumbe wa 'nenda kapumzike, umemaliza kazi yako'.

Mwili huo ulibebwa katika gari maalum la wazi la JWT ambalo liliendeshwa na wanajeshi huku pande zote kukiwa na pikipiki saba maalum za Jeshi la polisi.

Baada ya mwili huo kufikishwa katika Uwanja wa Uhuru, ulishushwa na kubebwa na maofisa wa jeshi wenye vyeo ya kanali pembeni wakiwapo maofisa wakuu wa JWTZ wenye vyeo vya brigedia Jenerali.

Baada ya mwili kuwekwa katika eneo lililokuwa limetengwa katika uwanja huo wilayani Temeke jijini Dar es Salaam, ratiba ya Ibada ya Misa maalum ilianza. Ibada hiyo iliongozwa na maaskofu watatu wa Kanisa Katoliki akiwamo Askofu wa Jimbo la Iringa, Tarcisius Ngalalekumtwa. Maaskofu wengine ni wa Jimbo la Tanga, Anthony Banzi na Askofu wa Jimbo la Mahenge, Agapitus Ndorobo.

**ASKOFU NGALALEKUMTWA**

Askofu Ngalalekumtwa alisema Mkapa alitoa mchango mkubwa katika nchi hususani katika mageuzi ya kiuchumi, hivyo kuna haja ya kila mtu kujifunza kutoka kwake.

Pia, alisema kuna haja ya kila mtu kusoma kitabu chake alichokizindua mwaka jana cha 'My Life, My Purpose (Maisha Yangu, Kusudio Langu) ili kila mtu ajifunze yale yaliyopo katika kitabu hicho.

Kwa mujibu wa Askofu huyo, sadaka iliyopatikana katika ibada maalum ya kuaga mwili wake jana, kwa maelekezo ya Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Yuda Tadei Ruwai'ch, itatumika kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za mapadre wa Parokia ya Lupaso kwa kuwa wakati wa uhai wake, Mkapa aliahidi kukarabati nyumba hizo kwa Sh. milioni 20, lakini bado hakuwa ametimiza.

**KUAGA MWILI**

Baada ya kumalizika kwa ibada, saa tano na nusu asubuhi,kazi ya kuaga mwili ilianza kwa wakianza viongozi wakuu wa nchi wakifuatiwa na wananchi hadi usiku.

**WATU WAZIMIA**

Baadhi ya wananchi waliopita kuaga mwili walizimia na kusaidiwa na wanajeshi pamoja na watu wa vyombo vya ulinzi na usalama waliokuwapo katika eneo hilo.

**ALICHAGUA PA KUZIKWA**

Mkuu wa ukoo wa kina Mkapa, Chifu Mkanona, alisema wakati wa uhai wake, alichagua kwamba endapo atafariki azikwe katika eno hilo.

Aidha, alisema eneo hilo ndilo limekuwa likitumika kuzika ndugu wa familia.

Alisema kufariki kwa Mkapa kumeacha giza kwa familia, kwa wana-Masasi na wananchi wote wa mikoa ya Kusini.

"Tunajisikia tuko gizani kwa sasa, Mkapa alitufanya tujisikie na sisi ni wa thamani, alitufanya tuonekane wa thamani tumepata thamani sababu yake," alisema na kuongeza:

"Kwa hivyo ameondoka tuna masikitiko makubwa sana na sijui kama uthamani huu utaendelea, sisi machinga wote huku tulipata thamani hiyo kwa sababu yake."



Rais John Magufuli akiingia katika uwanja wa Uhuru, wakati wa Misa ya kuuaga mwili wa Rais mstaafu, Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Taasisi yake yamwelezea kwa undani

**Na Elizabeth Zaya**

MTENDAJI Mkuu wa Taasisi ya Benjamini Mkapa, Dk. Ellen Senkoro, amesema wanaamini kwamba taasisi hiyo itaendelea kuwa imara kujiendesha kutokana na misingi imara iliyokuwa imejengwa na Rais mstaafu, Benjamini Mkapa ambaye ndiye mwanzilishi wake.

Dk. Senkoro alisema tangu Mkapa alipoanzisha taasisi hiyo, aliiwekea misingi imara na bora ya kujiendesha ambayo iliisaidia kusimama na kujiendesha yenyewe bila yeye kutoa fedha yake ya mfukoni.

"Tunashukuru kwamba tangu Mzee Mkapa aanzishe taasisi hii na kuiwekea misingi imara na bora ya kujiendesha, hajawahi kutoa fedha yake ya mfukoni na haijawahi kutetereka, shughuli zote za kuiendesha zimekuwa zikifanywa na Bodi kwa kushirikiana na Menejimenti, kwa hiyo tunamshukuru kwamba alituwekea mifumo na misingi mizuri,"alisema Dk. Senkoro.

Dk. Senkoro alisema lengo kuu la Mkapa kuanzisha taasisi hiyo ilikuwa ni kuimarisha afya za wananchi hususani walioko vijijini.

"Na hilo tumeweza kufanikiwa zaidi hasa wakati mzee yuko hai na kikubwa tulichojifunza kwake alitaka taasisi ijiendeshe yenyewe,"alisema Dk. Senkoro.

Alisema Mkapa alihakikisha kwamba inaundwa Katiba na mifumo mizuri kwa ajili ya kuisaidia taasisi hiyo kujiendesha yenyewe tangu awali.

"Tulijua kwamba ipo siku mzee ataondoka kwa sababu binadamu hatuishi milele na ndiyo maana akaweka misingi bora ya namna ya kuendesha taasisi yetu ikiwamo kuweka hiyo Katiba na mifumo mingine,"alisema Dk.Senkoro.

## Kilichosababisha kifo cha Mkapa

**Na Salome Kitomari**

FAMILIA ya Rais mstaafu wa serikali ya awamu ya tatu, Hayati Mzee Benjamin Mkapa (81), imeeleza sababu za kifo chake kuwa ni mshtuko wa moyo.

Familia ilieleza jana katika ufafanuzi wake kuwa Mzee Mkapa alipata mshtuko wa moyo baada ya kuugua malaria kwa siku mbili na kulazwa hospitalini.

Msemaji wa Familia, William Erio, akitoa taarifa wakati wa Misa Takatifu ya kuaga mwili wa Mzee Mkapa, alisema kumekuwa na uzushi mwingi kwenye mitandao ya kijamii, na kwamba ukweli ni kuwa alipata mshtuko wa moyo akiwa amekaa.

"Sababu ya kifo chake ni mshtuko wa moyo...nilidhani ni vizuri tuliseme maana kumeanza kuwa na maneno na maelezo ya kila mtu akijifanya ni mwelewa, nabii katika mitandao ya kijamii na katika sehemu nyingine," alisema Erio na kuongeza:

"Niwaombe na kuwasihi Watanzania wenzangu, tumuenzi Mzee wetu aliyetangulia mbele ya haki kwa kuheshimu ukweli huu."

Alisema: "Mzee wetu (Mkapa) alikuwa hajisikii vizuri akaenda hospitali baada ya kuchukuliwa vipimo alionekana ana malaria, akaanza matibabu akalazwa Jumatano na Alhamisi mchana aliendelea vizuri."

"Nilikuwa naye hadi saa mbili usiku akanipa maelekezo ya kumpelekea Baba Askofu Eusebius Nzigilwa (Askofu wa Jimbo Katoliki la Mpanda) kwamba alimkubalia atashiriki shughuli ya kumuaaga (Askofu) jana, ila hataweza kuhudhuria, akaniambia nimfikishie salamu na bahasha yake."

Kwa mujibu wa Erio, alimuacha Mkapa akiangalia lunigha iliyokuwa inaonyesha matukio mubashara ya wagombea waliokuwa wanaomba uteuzi wa kupeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi kupitia Umoja wa Wanawake wa chama hicho (UWT).

"Niliagana naye kwenda kutekeleza alichoniagiza nikiwa na wana familia wengine...baada ya kusikiliza taarifa ya habari aliinuka akitaka kutoka, alipoinuka kukaa aliinamisha kichwa na walipokuja (madaktari) kumpima walithibitisha amefariki," alibainisha Erio ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Mkapa alifariki usiku wa kuamkia Ijumaa (Julai 24) na msiba wake kutangazwa rasmi usiku huo huo na Rais John Magufuli kupitia vyombo vya habari.

Hayati Mkapa ameacha mjane Anna Mkapa na watoto wawili.

Aliiongoza Tanzania kuanzia mwaka 1995 (ulivyoanza mfumo wa vyama vingi) hadi 2005, huku akiacha alama ya ukweli na uwazi, mapambano dhidi ya rushwa.

Pia kuanzisha Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACADIS), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mfuko wa Barabara na Mtuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kwa kutaja baadhi.

## MKAPA 1938 - 2020



Waimbaji wa kwaya ya Kanisa Katoliki, wakiimba nyimbo za maombolezi wakati wa Misa ya kuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, katika Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mataifa yamlilia Mzee Mkapa

**Salome Kitomari na Elizabeth Zaya**

VIONGOZI mbalimbali duniani wamemlilia hayati Benjamini Mkapa, kwa kumwelezea kama mwanademokrasia aliyeiwezesha Tanzania kukua kiuchumi.

Katika kurasa za Twiter za viongozi hao, kila mmoja alimwelezea Mkapa kwa jinsi alivyomfahamu, kama Rais wa Rwanda, Paul Kagame, aliandika "Tumeshtushwa na kifo cha rais Mkapa, tunatoa salamu zetu za rambirabi kwa familia yake, watu wa Tanzania na rafiki tangu Rais John Magufuli."

"Kwa kumpoteza kaka yetu Mkapa ni maumivu kwa bara zima la Afrika, alikuwa muumini wa umajumuni wa Afrika ambaye mchango wake ulionekana vyema Tanzania," alisema.

Katibu Msaidizi wa Masuala ya Afrika wa Marekani, Balozi Tibor Bagy, aliyesema; "Tunatoa salamu zetu za rambirambi kutoka mioyoni mwetu kufuatia kifo cha aliyekuwa rais wa Tanzania, Benjamini Mkapa, rafiki mkubwa wa Marekani, tunakumbuka jitihada zake za kuinua demokrasia na kuimarisha taasisi Tanzania, pamoja na kuchangia amani na usalama barani Afrika."

Naye Balozi wa Canada nchini, Pamela O'Donnell aliandika "Tumepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha Rais Mkapa. Atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa kwa nchi ya Tanzania, lakini pia Canada kwa utumishi wake akiwa Balozi wa Tanzania, tunatoa pole kwa familia yake na Watanzania kwa ujumla."

Katika ukurasa wa Twiter wa Mahakama ya Afrika, waliandika: "Tunaomboleza, Bendera ya Tanzania, Mahakama ya Afrika na Umoja wa Afrika (AU) jijini Arusha zitapepea nusu mlingoti kuomboleza kifo cha Rais Benjamin Mkapa."

Naye Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, aliandika "Ni majonzi makubwa kwa kifo cha Rais Benjamin Mkapa. Nilianza kufanya naye kazi mwaka 1967 tukiwa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Makerere na alikuwa Mhariri Mkuu wa gazeti la Nationalist."

Alisema Makapa alivyokuwa Rais wa Tanzania walifanya kazi kwa karibu kuimarisha muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). "Afrika imepoteza mtu muhimu sana, Apumzike kwa amani."

"Nitatuma salamu za rambirambi za zangu na watu wa Uganda kwa Mama Anna Mkapa, watoto na Watanzania. Bendera ya Uganda itapepea nusu mlingoti kwa siku tatu kuanzia jana saa 12 jioni," alisema.

Pia, Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta Juzi alitangaza maombolezo ya siku tatu nchini humo kumlilia Rais Mkapa, huku akielezea jitihada zake za kuleta amani nchini humo.

# Mabalozi: Tanzania, Afrika imepoteza msuluhishi nguli

**Na Mwandishi Wetu**

MABALOZI mbalimbali wanaowakilisha nchi zao hapa nchini, wameendelea kusaini kitabu cha maombolezo nyumbani kwa Rais mstaafu wa Tanzania, Benjamin Mkapa na kumuelezea kuwa ni kiongozi mahiri na msuluhishi nguli wa amani barani Afrika na duniani.

Baadhi ya mabalozi hao walieleza walivyoguswa na msiba wa Mkapa na kusema Tanzania imepoteza kiongozi na msuluhishi nguli wa amani barani Afrika na duniani.

Kwa upande wake, Balozi wa Zambia nchini, Benson Keith Chali, amesema Zambia wameguswa na msiba kwa kuwa Tanzania na Zambia ni ndugu, "toka mwanzoni Nyerere na Kaunda walikuwa ndugu na sisi tumeendelea kuwa ndugu na unapopoteza ndugu unaumia sana. Sisi kama Zambia kwa kweli tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha mzee Mkapa."

"Tutamkumbuka mzee Mkapa kama kiongozi aliyesimamia amani maeneo mbalimbali barani Afrika ikiwamo Kenya, Burundi, Congo DRC na kwingineko duniani," alisema Chali na kuongeza

"Sisi kama Zambia tunatoa sana pole kwa familia yake, Serikali ya Tanzania na Watanzania kwa ujumla ...tunaomboleza wote msiba huu mzito."

Naye Balozi wa Denmark nchini, Mette Dissing-Spandet, alisema kuwa Rais mstaafu Mzee Mkapa alikuwa kiongozi mahiri kwa Tanzania, pia rafiki na mfano wa kuigwa na mataifa mbalimbali.

"Kwetu sisi kama Denmark alikuwa rafiki na tutaendelea kumkumbuka daima kwa upendo wake," alisema Mette.

Balozi wa Algeria nchini, Ahmed Djellal, alisema mzee Mkapa alikuwa mtetezi wa amani barani Afrika na atakumbukwa kwa mema aliyoyafanya kwa kuwa aliyafanya kwa jitihada na weledi wa hali ya juu, Mungu ampumzishe kwa amani.

# ... Sekta binafsi kumkumbuka kwa mambo sita

**Na Mwandishi Wetu**

CHEMBA ya Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA), imetaja mambo makuu sita yaliyofanywa na Rais mstaafu Benjamin Mkapa, wakati wa uongozi wake, ambayo yamesaidia ukuaji wa sekta binafsi nchini.

Mkapa (81), aliyeliongoza taifa kama Rais wa Awamu ya Tatu (1995-2005), alifariki dunia usiku wa kuamkia Ijumaa hospitalini jijini Dar es Salaam alikokuwa akipatiwa matibabu. Kifo chake kilitangazwa na Rais John Magufuli usiku huo.

Akitaja michango ya Mkapa kwa sekta binafsi nchini, Rais wa TCCIA, Paul Koyi, alisema jana kuwa, kiongozi huyo alikuwa muumini wa sekta binafsi na aliamini sekta hiyo ni muhimili na injini ya ukuaji wa uchumi.

Koyi alisema kwamba ni Mkapa aliyefungua uchumi na kuruhusu sekta binafsi kuwekeza na kushamiri katika sekta na nyanja mbalimbali za kiuchumi nchini.

Koyi pia alisema Mkapa aliishi maneno yake na imani yake kwa sekta binafsi kwa kuunda mfumo wa majadiliano wa uwapo wa sekta binafsi, kukiundwa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) mwaka 1998 na Baraza la Biashara la Taifa (TNBC) mwaka 2001 ambalo Mkapa alikuwa Mwenyekiti wake wa kwanza.

"Uundwaji wa Baraza la Biashara la Taifa ulilenga kuratibu majadiliano baina ya sekta ya umma na binafsi kuhusu sera, sheria na kanuni zinazosimamia biashara na uwekezaji nchini, ili kuchochea ushiriki wa sekta binafsi katika kuleta maendeleo na kukuza uchumi," alisema Koyi.

Koyi alisema mchango mwingine, Mkapa alifanikisha kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mapato kwa kuunganisha idara za kodi za ndani, mauzo na forodha, hivyo kuleta ufanisi na urahisi wa ulipaji kodi na kuongeza mapato ya serikali.

Alisema Mkapa katika kipindi chake, alihamasisha uanzishwaji wa vyama vya biashara vya kisekta nchini kwa lengo la kusimamia maslahi ya kampuni na biashara zao.

Alisema hakuishia hapo, bali alishauri sekta binafsi za Afrika Mashariki kuungana ili kujadili masuala yahusuyo mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji ndani ya ukanda huo ambapo Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC) lilianzishwa mwaka 1997.

"Mkapa pia alikuwa kiongozi wa kwanza kukubali na kuruhusu dhana hii ya ushirikiano baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma kupitia miradi ya Ubia (Public Private Partnership)," alikumbusha Koyi.

Alisema Bodi ya Wakurugenzi ya TCCIA, imesikitishwa na taarifa za kifo cha Rais huyo mstaafu ambaye alikuwa mwanachama wa kudumu wa chemba hiyo.

"TCCIA kama sehemu moja ya mihimili ya sekta binafsi, tumepoteza kiongozi shupavu, mwanadiplomasia mahiri na mmoja wa waasisi wa maendeleo ya sekta binafsi nchini na mwanachama wetu wa maisha," alisema Koyi.



Wachuuzi wa maziwa wakiwa wamepaki bidhaa hiyo kwenye chupa katika eneo la Kwa Matiasi Kibaha, Pwani. **PICHA:MIRAJI MSALA**

# Wamuenzi Mkapa ujenzi mradi maji Ziwa Victoria

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAJUMBE wa bodi ya maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Shinyanga (SHUWASA),wamemuezi Rais mstaafu wa awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa, kwa kutekeleza mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria na kuyapeleka mkoani Shinyanga.

Mradi huo uliopo katika Kijiji cha Ihelele wilayani Misungwi mkoani Mwanza, ulianza kutekelezwa mwaka 2003 chini ya Mzee Mkapa na ulikamilika mwaka 2008 ambapo 2009 ulianza kusukuma maji mkoani Shinyanga, huku waziri wa maji kipindi hicho akiwa Edward Lowassa.

Mwenyekiti wa Bodi ya SHUWASA, Mwamvua Jilumbi, alibainisha hayo juzi, wakati wajumbe wa bodi hiyo walipofanya ziara ya kutembelea mradi huo kutoka ndani ya Ziwa Victoria na kupelekwa Shinyanga na mikoa ya jirani.

Alisema wananchi wa mkoa wa Shinyanga wanamuezi Mkapa, kwa kuwatekelezea mradi mkubwa wa majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria, kitu ambacho hakikuwa rahisi, lakini kwake alitekeleza na hatimaye kuondoa kero ya uhaba wa maji mkoani humo.

"Tunatuma salama za pole kwa Rais John Magufuli kwa kuondokewa na Rais mstaafu Benjamini Mkapa, ambaye sisi wana-Shinyanga tutamkumbuka na kumuenzi kwa kutekelezea mradi mkubwa wa maji kutoka ndani ya Ziwa Victoria na kuyaleta hapa Shinyanga, na sasa hatuna shida ya maji tena," alisema Jilumbi.

Naye Mkurugenzi wa SHUWASA, Flaviana Kifizi, alisema wamefanya ziara hiyo na wajumbe wa bodi ya maji, ambapo ni wapya ili kujua sehemu halisi ya chanzo cha maji hayo kutoka Ziwa Victoria namna yanavyozalishwa hadi kumfikia mwananchi.

Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama na Shinyanga (KASHWASA), John Nzengo, alisema wao ndio wazalishaji wakuu wa maji hayo kutoka ndani ya Ziwa Victoria, na kuyauza kwenye malmlaka zingine za maji, mna kuwa mradi huo umeondoa kabisa changamoto ya ukosefu wa maji Shinyanga.

Aidha, alisema ujenzi wa mradi huo ulianza mwaka 2003 chini ya uongozi wa Hayati Mkapa, na ulikamilika mwaka 2008 ambapo 2009 ulianza kuzalisha maji kutoka Ziwa Victoria na kuyasambaza mkoani Shinyanga, na sasa mradi unatoa huduma na mikoa mingine ukiwamo Tabora.


IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL
FOR MARA AT MUSOMA

MISC. APPLICATION NO. 124 & 125 OF 2020

FIDELIS JULIUS CHACHA..............................................APPLICANT

VERSUS

1. CHACHA JULIUS MWITA
2. SHADRACK MALIBWA ................................RESPONDENT
3. JOHNSON HARUN

SUMMONS/ NOTICE

TO,
1. CHACHA JULIUS MWITA
2. SHADRACK MALIBWA
3. JOHNSON HARUN

The above mentioned applicant has instituted a suit in this Tribunal, against you, particulars of which are mentioned in a copy of the Application which is obtainable from the registry of this Tribunal,

**YOU ARE HEREBY SUMMONED TO APPEAR IN THIS TRIBUNAL** in person (s) or by recognized agent (s) for mention on 03rd August, 2020 at 08:00am in the fore noon.

**TAKE NOTICE THAT;**

In default of your appearance on the said day, the above mentioned suit shall be mentioned and determined in your absence.

Give under my hand and seal of this Tribunal this.......10th.......day of ......JUNE...., 2020.

Kitungulu Elias
Chairman
The District Land and Housing Tribunal – Mara


# Msajili avipa neno vyama vya siasa

**Na Futuna Seleman**

MSAJILI Msaidizi wa Vyama Vya Siasa nchini, Sixty Nyahoza, amevitaka vyama hivyo vikipata bahati wagombea wao kupitishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu, wazingatie sheria katika kampeni.

Nyahoza aliyasema hayo katika mkutano mkuu maalum wa Chama cha Sauti ya Umma (SAU) uliowashirikisha wanachama ambao ni wajumbe wa kamati kuu ya chama hicho, akiwa mgeni mwalikwa.

"Nimefurahishwa SAU imejiandaa vizuri kwa mujibu wa sheria, mkipata bahati wagombea kuteuliwa na Tume mtii sheria na maadili yaliyowekwa, tunapenda kampeni zenu ziwe za kistaarabu," alisema.

Alisema kama mlezi wa chama hicho hatarajii SAU kuvunja sheria kwa vile anakifahamu kwa kufanya kampeni za kistaarabu

Alivitaka watia nia wa vyama wasitoe rushwa ili wapitishwe, na wakishateuliwa na Tume wasitoe rushwa ili washinde.

"Wagombea wa SAU epukeni rushwa, viongozi wapeni adhabu watakaobainka kutoa rushwa kemeeni rushwa kwa nguvu zote, tunategemea taasisi nyingine za serikali kusimamia vitendo vya rushwa ikiwamo ofisi yangu," alisema.

# DP yapitisha majina wagombea urais, yataka haki kutendeka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Democractic Part (DP), kimepitisha majina ya wanachama awatakaokiwakilisha katika uchaguzi mkuu 2020, kwa nafasi ya Urais wa Jamuhuri ya Muungano Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Majina ya wateule hao yalitangazwa jana na Katibu Mkuu wa DP, Abdul Mluya, katika mkutano mkuu maalum wa kufanya uteuzi wa majina ya wagombea wa nafasi mbalimbali.

Mluya, alisema wamemchagua Philipo Fumbo, kuipeperusha bendera ya chama hicho katika kinyang'anyiro cha nafasi ya urais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia, wamemchagua Zainabu Juma Hamisi, kuwa mgombea mweza.

"Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chama chetu cha DP, kimemteua kwa kauli moja ndugu Shaffi Hassani Suleimani, ambaye atakwenda kupambana na Mwinyi katika nafasi ya urais Zanzibar," alisema Mluya.

Alisema, katika uchaguzi wa mwaka huu chama hicho kimejipanga kuhakikisha kuwa kinavunja rekodi kwa kushika dola, katika serikali zote mbili bara pamoja na visiwani.

"Ilani yetu ni tamu sana, wagombea wetu watakwenda kuiuza na itauzika vizuri sana na tutashinda katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu," alisema Mluya.

Vile vile, alitaja kaulimbiu yao mwaka huu, katika uchaguzi mkuu ni 'Hakuna kushinda bila kupingwa', kwkakua wataweka wagombe kila eneo kuanzia urais, ubunge pamoja na udiwani.

"Tunaiomba Tume ya Taifa ya uchaguzi NEC, kuhakikisha kuwa inatutangaza kuwa washindi bila kubadili chochote na kama tutakuwa tumeshindwa kihalali basi tutangazwe pia kuwa tumeshindwa katika uchaguzi," alisema.

Alisema, kama watadhulumiwa katika uchaguzi huu kama kawaida yao lazima waende mahakamani ili kupata haki yao.

"Watu wanasema DP inapenda sana kesi tunawaambia kuwa kama tutadhulumiwa haki yetu katika uchaguzi mkuu mwaka huu, lazima twende mahakamani hata kama tutakuwa na kesi 100," alisema Mluya.

Pamoja na kuchagua majina ya wanachama watakao wakilisha katika nafasi hizo kubwa, pia mkutano huo ulipitisha marekebisho ya katiba ili kuendana na mabadailiko ya sheria mpya ya vyama vya siasa.

Mteule katika nafasi ya urais Zanzibar, Suleimani, alisema kuwa anawashukuru wajumbe kwa kumpa ridhaa hiyo na atahakikisha kuwa chama chake kinashinda katika uchaguzi mkuu 2020.

"Kama nikipata nafasi ya kuwa Rais wa Zanzibar basi nitahakikisha kuwa bahari tuliyonayo inakuwa kitega uchumi chetu kikubwa ambacho kitasaidia kuongeza pato la taifa kwa kubuni miradi mbalimbali," alisema.

# Mtiania udiwani adondosha 'kibuyu' akiingia ukumbini

**Na Jumbe Ismailly, IGUNGA**

MMOJA wa wagombea wa kiti cha udiwani wa Kata ya Sungwizi, wilayani Igunga, Katambi Sospeter, amejikuta katika wakati mgumu baada ya kuangusha kibuyu kilichokuwa na dawa akiingia kwenye ukumbi wa kupigia kura za maoni Shule ya Msingi Sungwizi.

Sospeter ambaye pia ni Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), alipatwa na mkasa huo juzi wakati alipokuwa akipanda ngazi kuelekea ukumbi wa kupigia kura hizo.

Wakati akiwa katika harakati za kuingia ukumbini, kibuyu hicho kilichodhaniwa kuwa na dawa kilichomoka kutoka kwenye mfuko wake wa suruali na kudondoka mbele ya baadhi ya wajumbe waliokuwapo kwenye jengo hilo.

Kwa mujibu wa baadhi ya wajumbe waliohudhuria kikao hicho cha kura za maoni, akiwamo Therezia Bleck, walimwambia mgombea huyo kuwa ameangusha kibuyu ndipo aposhikwa na bumbuwazi na kubaki amesimama bila kuangalia alipokuwa akiitwa.

Baada ya dakika 10, mjumbe Bleck alichukua kibuyu hicho na kumkabidhi mgombea huyo huku askari wawili wa jeshi la akiba waliokuwa wakiimarisha ulinzi kwenye eneo hilo, wakimhoji kuhusu kibuyu hicho cha dawa katika kura za maoni.

Mgombe huyo alikiri kibuyu hicho ni mali yake na kujitetea kuwa amezaliwa mapacha hivyo kiutaratibu inatakiwa awe na kibuyu cha dawa wakati wote.

Licha ya kujieleza na kujitetea, askari hao walimzuia kuingia na kibuyu hicho kwenye ukumbi wa kupigia kura na kumtaka akikabidhi kwa askari hao mpaka atakapomaliza kura za maoni ndipo wamrudishie, ushauri ambao hata hivyo hakukubaliana nao.

Katika majadiliano yalichukua kama dakika 30, mgombea huyo alipoamua kukipeleka kibuyu hicho nyumbani na kurudi kupigia kura.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Sungwizi, Emmanuel Mpya, alithibitisha mgombea huyo kuangusha kibuyu cha dawa na kwamba kitendo hicho hakikumfurahisha.

Alimuonya mgombea huyo kutorudia tena tabia hiyo.

Msimamizi Ramadhani Omari, alitangaza matokeo ambayo yalionyesha Njeri Ibrahim kupata kura 21, Katambi Sospeter aliyedondosha kibuyu kupata kura 22 na Diwani aliyemaliza muda wake, Matikiti Gaspar aliongoza kwa kura 62.

Hivi karibuni katika mkutano wa kura za maoni Jimbo la Igunga, Mbunge aliyemaliza muda wake, Dk. Peter Kafumu, alianguka ghafla alipokuwa akiombewa kanisani kabla ya kwenda kuingia kwenye ukumbi wa mikutano wa Sakao, mjini Igunga.

Matokeo ya kura za maoni katika jimbo la Igunga ni kwamba Kabeho Henry Charles alipata kura 202, Kashaga Anwar Rwehumbiza alipata kura 166 na Dk. Kafumu alipata kura 56.

# SAU yataja watakaogombea urais Zanzibar na Bara

**Na Futuna Seleman**

CHAMA cha Sauti ya Umma (SAU) kimemteua, Mtamegwa Mgwaya kuwa mgombea urais kupitia tiketi ya chama hicho upande wa Tanzania Bara huku Issa Mohamed Zonga kuwa mgombea nafasi hiyo Visiwani katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu.

Akiwatambulisha wateule hao kwa wanachama na viongozi wengine wa kamati kuu kupitia Mkutano Mkuu Maalum wa chama taifa, Mwenyekiti wa SAU, Bertha Mpata, alisema wagombea wa chama hicho kwa Bara na Zanzibar wataambatana na mgombea wenza ambao ni kinamama na kuwataka kusimamia taratibu za vyama ili kuondoa vurugu.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Majalio Kyara, alisema waliotia nia walikuwa watano na waliochukua fomu ni wawili, mmoja alijitoa na chama kilimpitisha.

"Natoa rai kwa wataopitishwa na Tume ya Uchaguzi wafanye kampeni kwa utulivu na amani kwa kuzinadi sera za chama, wanachama kuwa na weledi na siku ya uchaguzi baada ya kumaliza kupiga kura kila mtu arejee nyumbani kusubiri matokeo ili kuepusha mikusanyiko inayoweza kusababisha kuvunjika kwa amani," alisema Kyara.

Aliupongeza uongozi wa serikali ya awamu ya tano kwa mambo mazuri iliyofanya na kwamba lengo la SAU ikishika madaraka ya kuongoza nchi ili ifike pazuri zaidi.

Mteule wa nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mgaywa, alisema kupitia uzoefu wake katika siasa atasimamia maadili ya vyama wakati wote wa mchakato kwa kuwa SAU haipo kwa ajili ya upinzani pekee bali imelenga uamuzi unaofikiwa na chama hicho yaweze kufika Ikulu na kuleta mabadiliko.

"Rais Magufuli pamoja na kuwa kuna changamoto kadhaa amejitahidi sana na chama cha SAU kitakaposhika dola kitakuwa ni mbadala wa CCM na si upinzani," alisisitiza Mgaywa.

Mgombea nafasi hiyo kwa upande wa Zanzibar Zonga, alisema chama cha SAU kinakubalika visiwani humo na atakapopata nafasi atasimamia misingi yote iliyotolewa na Tume na Ofisi ya Msajili.

Mgombea mwenza, Satia Sebwa, alisema atahakikisha anasimamia misingi yote ya chama wakati wote wa mchakato wa kuelekea uchaguzi na ilani zote za chama hicho.

Msajili Msaidizi wa vyama vya siasa, Sisty Nyahoza, alivitaka vyama vya siasa kuacha kujihusisha na vitendo vya rushwa ili kuendelea kulinda nidhamu ya vyama vyao.

Alisema endapo watia nia watachaguliwa na Tume ya uchaguzi wahakikishe wanafuata maadili yanayotakiwa ya vyama vya siasa.

Alikipongeza chama hicho kwa kuwa mstari wa mbele kufuata taratibu, kanuni na maadili yanayopaswa kufanywa na vyama vya siasa.

**The United Republic of Tanzania**
**MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM**

## TAARIFA KWA UMMA

Moja ya jukumu la Wizara kupitia Sheria ya utalii Na. 29 ya Mwaka 2008 ni kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora. Mfumo unaotumika katika kutekeleza kazi hii ni ule ulioandaliwa na kukubalika na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambao unafuata vigezo vya ubora wa kimataifa. Kulingana na vigezo hivyo, kiwango cha juu cha ubora ni daraja la nyota 5 (five star) na kiwango cha chini ni daraja la nyota 1 (one star). Aidha, huduma za malazi ambazo hazijafikia kiwango cha daraja la nyota hutambulika kama huduma zilizothibitishwa (Approved Accommodation Facilities).

Wizara inapenda kuutaarifu Umma kuwa kazi ya kukagua na kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora iliyofanyika Jijini Dodoma imekamilika, ambapo huduma za malazi 24 zimepata viwango mbalimbali vya ubora kama ifuatavyo:

| Na. | Jina | Aina ya Huduma za Malazi | Daraja La Ubora |
|---|---|---|---|
| 1. | New Dodoma Hotel Ltd | Hoteli ya Mjini | Nyota Tatu |
| 2. | Nashera Hotel | Hoteli ya Mjini | Nyota Tatu |
| 3. | Fantasy Village Hotel | Hoteli ya Mjini | Nyota Tatu |
| 4. | Morena Hotel | Hoteli ya Mjini | Nyota Mbili |
| 5. | St. Gasper Hotel and Conference Centre | Hoteli ya Mjini | Nyota Mbili |
| 6. | African Dream | Hoteli ya Mjini | Nyota Mbili |
| 7. | Royal Village Hotel | Hoteli ya Mjini | Nyota Mbili |
| 8. | Mesuma Lodge | Hoteli ya Mjini | Nyota Mbili |
| 9. | Nala Centurion Hotel | Hoteli ya Mjini | Nyota Moja |
| 10 | Hotel Kitemba | Hoteli ya Mjini | Nyota Moja |
| 11 | Four Points Hotel | Hoteli ya Mjini | Nyota Moja |
| 12 | Modern Hotel | Hoteli ya Mjini | Iliyothibitishwa A |
| 13 | City Boys Hotel | Hoteli ya Mjini | Iliyothibitishwa A |
| 14 | City Climax Hotel | Hoteli ya Mjini | Iliyothibitishwa A |
| 15 | Giftland Hotel | Hoteli ya Mjini | Iliyothibitishwa A |
| 16 | Dear Mama | Hoteli ya Mjini | Iliyothibitishwa A |
| 17 | Nam Hotel | Hoteli ya Mjini | Iliyothibitishwa A |
| 18 | Gold Coins Hotel | Hoteli ya Mjini | Iliyothibitishwa A |
| 19 | Summit Hotel | Hoteli ya Mjini | Iliyothibitishwa A |
| 20 | Magdon Lodge | Hoteli ya Mjini | Iliyothibitishwa B |
| 21 | Munich Hotel | Hoteli ya Mjini | Iliyothibitishwa B |
| 22 | Johanic Hotel | Hoteli ya Mjini | Iliyothibitishwa B |
| 23 | Domiya Hotel | Hoteli ya Mjini | Iliyothibitishwa B |
| 24 | Dodoma Rock 2010 Hotel | Hoteli ya Mjini | Iliyothibitishwa B |

Ninawapongeza wamiliki wote wa huduma za malazi Jijini Dodoma kwa kutunukiwa daraja za ubora na ninatoa rai kwa wamiliki wengine wa huduma hizo kuboresha hoteli pamoja na huduma wanazotoa ili kufikia daraja za juu. Ni imani yangu kuwa kazi hii ya upangaji wa huduma za malazi katika daraja za ubora itasaidia kuongeza ubora wa huduma zitolewazo katika Sekta ya Utalii nchini na hivyo kuifanya nchi yetu iweze kushindana kimataifa.

Kwa maelezo zaidi tafadhali tembelea tovuti yetu www.maliasili.go.tz au tembelea ofisi za Wizara, Idara ya Utalii zilizopo katika Jengo la Chuo Kikuu cha Dodoma na Ofisi za Utalii za Kanda zilizopo katika Jengo la Mpingo, Dar es Salaam; Jengo la PSSSF, Mwanza; Jengo la NSSF, Iringa na TANAPA Makao Makuu, Arusha.

Imetolewa na:
KATIBU MKUU
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
Simu: +255 22 2864271/2864230
Barua pepe: ps@maliasili.go.tz
06 Juni, 2020

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Marekebisho mapya kanuni Ligi Bara yatazamwe sasa

**HATIMAYE** Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Daraja la Kwanza na ile ya Daraja la Pili zimefikia kileleni jana baada ya msimu mgumu zaidi kuwahi kutokea nchini.

Tunasema msimu mgumu hasa kutokana na ushindani mkubwa wa kupata timu za kushuka daraja na za kucheza mechi za mchujo kubaki Ligi Kuu msimu ujao, lakini pia kinyang'anyiro cha nafasi ya pili kati ya Yanga na Azam FC.

Nafasi hizo zilihitaji hadi mechi za mwisho kuchezwa jana ili kujua hatma ya nani anakuwa wapi katika msimamo wa ligi hiyo msimu huu.

Lakini kubwa na lililotikisa ligi hizo msimu huu kama ilivyokuwa nyingine duniani, ni kutokana na kusimama kwa kipindi cha takriban miezi mitatu baada ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19.

Ugonjwa huo ambao husababishwa na virusi vya corona, uliotangazwa na Shirika la Afya duniani (WHO), kuwa janga la kimataifa, ulisababisha ligi nchini kusimama zikiwa zimebaki raundi 10 msimu kumalizika.

Tulishuhudia baadhi ya ligi za mataifa mengine hususan barani Ulaya kama Ufaransa, Uholanzi na Ubelgiji ligi zao zikifutwa kabla ya msimu kumalizika, lakini bingwa na wawakilishi wa michuano ya kimataifa wakipatikana.

Si hilo tu, bali kwa baadhi pia mabingwa wa ligi msimu huu walifahamika, hiyo ikitokana na kuwapo kwa kanuni zinazoruhusu bodi zao za ligi ama mashirikisho kufanya hivyo pindi panapotokea majanga kama hayo na ligi kufutwa.

Hilo pia lilifanyika kwa majirani zetu, Kenya ambao walilazimika kufuta ligi zao huku ikiwatangaza wawakilishi wa michuano ya kimataifa kutokana na kuwapo kwa kanuni.

Lakini Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na Bodi ya Ligi nchini (TPLB), walishikwa na kigugumizi kizito wakisugua kichwa wachukue uamuzi gani kumpata bingwa ama wawakilishi wa nchi kwenye mashindano ya kimataifa kutokana na kutokuwapo kwa kanuni.

Shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, aliyeonyesha ujasiri wake wa kuliongoza Taifa kupambana na corona na maambukizi kupungua kwa kiasi kikubwa hatua iliyomfanya kuruhusu ligi hizo tatu nchini kuendelea kwa tahadhari kuchukuliwa.

Hiyo ndiyo iliyokuwa ahueni kwa TFF na TPLB kwa ligi hizo kumalizika rasmi jana kwa mabingwa, wakilishi wa michuano ya kimataifa kujulikana pamoja na zile za kushuka daraja moja kwa moja na za kupanda.

Kilichobaki sasa ni mechi za mchujo kujua timu mbili zitakazoungana na nyingine 16 kucheza Ligi Kuu msimu ujao lakini pia fainali ya Kombe la Shirikisho maarufu FA Cup kati ya Simba na Namungo FC.

Hata hivyo, kuelekea msimu mpya wa 2020-21, TFF pamoja na TPLB sasa hawana budi kuhakikisha kanuni za ligi zinafanyiwa marekebisho ikiwamo hiyo ya namna ya kumpata bingwa na wawakilishi wa michuano ya kimataifa endapo patatokea majanga kama hayo ya ligi kutomalizika.

Tunatambua yapo marekesho mengi yanayopaswa kufanywa, ikiwamo malalamiko ya klabu kutaka kanuni ya timu kuchukua mapato yote ya mechi za nyumbani kubadilishwa, hivyo TFF na TPLB hawana budi kukaa na wanachama wake sasa ili kuzitazama kabla ya msimu mpya kuanza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Tutoe maoni kanuni za Ligi tusije lalamika

Na Adam Fungamwango

**KUNA** baadhi ya wadau na mashabiki wa soka walikuwa wakihoji au kupinga kanuni za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20 ambao ulimalizika jana kwenye viwanja mbalimbali nchini.

Walikuwa wakikosoa, lakini ukiangalia sana wengi ukosoaji wao ulikuwa zaidi kwenye ushabiki wa klabu wanazozishabikia. Kanuni hizo zikiizigusa timu wanazoshabikia basi unazuka ubishi na kuanza kuulizana ni nani aliyetunga na kuleta kanuni hizo. Na kwa nini? Mbona ni kanuni mbovu?

Lakini wasichokijua mashabiki wengi wa soka ni kwamba, kanuni hizo zinaanza kutungwa na na wadau na kupelekwa kwenye Bodi ya Ligi ya Shirikisho la Soka Nchini (TFF) ambayo inachakata na kuzitoa rasmi. Kanuni hizi hupendekezwa na kupitishwa kila kabla ya msimu kuanza.

Tayari Bodi ya Ligi imetangaza au imefungua mchakato wa maboresho ya kanuni ya Ligi Kuu msimu ujao wa 2020/21. Pia zitatumika kwenye Ligi Daraja la Kwanza na la Pili.

Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Almasi Kasongo amesema kuwa kanuni hizo zinatakiwa ziwasilishwe mpaka Julai 31 ambapo utakuwa ndiyo mwisho wa kupokea maoni.

"Mpira ni mchezo pendwa, makundi mbalimbali yajitokeze kwa ajili ya kutoa maoni. Tayari tumeshaanza kupokea mapendekezo, tena kuna mwitikio mzuri tu." alisema Kasongo.

Akaongeza kuwa kumekuwa na changamoto kwenye kanuni za Ligi Kuu msimu uliomalizika jana, hivyo kuwataka wadau waharakishe kabla ya kwenda kuchakatwa na Kamati ya Utendaji.

"Kamati ya Utendaji inatarajia kukaa Agosti 2 mjini Sumbawanga kupitia kanuni hizo, ndiyo maana utaona mwisho wetu wa kupokea ni Julai 31 na si zaidi ya hapo," alisema.

Kwa maneno hayo ni kwamba makundi mbalimbali ambayo yanahusiana na mambo ya soka kama vile wachezaji, waamuzi, makocha, chama cha madaktari wa michezo, chama cha wachezaji wa soka nchini Sputanza, waandishi wa habari na wengineo wanatakiwa kuandika mapendekezo na kuyawasilisha.

Hii itaondoa manung'uniko pale kanuni hizo zitakapoanza kufanya kazi ya kuwaadhibu wachezaji, makocha, waamuzi na wengineo.

Kila makundi yataona yalishiriki kutoa maoni, hivyo hakuna kulaumiana.

Huko nyuma tumeona baadhi ya viongozi wa klabu za soka nchini wakikacha kutoa mapendekezo ya kanuni, badala yake zinapoanza kutumika wao wanaanza kulalamika na kuilaumu TFF pamoja na bodi kuwa wanaonewa.

Ikumbukwe kuwa msimu huu Ruvu shooting ilinyang'anywa pointi tatu na magoli matatu dhidi ya Prisons kwa kile kilichosemekana kuwa wenyeji hawakuwa na gari la wagonjwa. Hili lilikuwemo kwenye kanuni ya Ligi Kuu iliyopita, hivyo kama inaonekana kuwa haipendezi kuwepo msimu ujao basi mapendekezo yanatakiwa.

Kuna wakati baadhi ya mashabiki wa Yanga walikuwa wakilalamika juu ya kocha wao wa wakati huo, Mwinyi Zahera kuhukumiwa kutokana na nguo zake alizokuwa akivaa ambazo hazitakiwi kikanuni.

Huu ndiyo wakati wa kupeleka mapendekezo ya kutaka kuwe na ufafanuzi wa kina juu ya aina ya nguo za makocha kuvaa wanapokuwa kwenye benchi, siyo kusubiri adhabu zinatoka kwa mujibu wa kanuni ndiyo watu waibuke.

Lakini pia kuna kanuni inaopata wenyeji mapato yote ya mechi. Kanuni hii imeonekana kulalamikiwa na viongozi hasa wa klabu za Simba na Yanga, hivyo ni wajibu wao sasa kutaka zirekebishwe ili utaratibu urudi ule ule wa kugawana nusu kwa nusu.

Hayo ni baadhi ya mambo ambayo yalikuwa yakikosolewa sana na viongozi na mashabiki wengi wa soka msimu uliopita, sasa ni wakati wa kuandika maoni ya kutaka yarekebishwe, lakini pia kupendekeza mengine ambayo yanaweza kusaidia soka la Tanzania.

Mfano kuna wachezaji wanaocheza rafu za kutaka kumiza wenzao bila ya kuwa na mpira. Hawa inatakiwa hata kama wakipewa kadi nyekundu au hawajapewa, lakini adhabu zao ziwe angalau kukosa mechi tano na si tatu kama wanaocheza rafu zingine zinazostahili kadi nyekundu.

Kuna rafu za mpira zinazochezwa wakati wa kugombea mpira zinazostahili kadi nyekundu, lakini kuna kadi nyekundu zingine za wachezaji wanapiga wenzao bila ya kuwa na mpira, hizi inafaa ziongezwe na kufikia mechi tano na faini Sh. milioni mbili badala ya moja.

# MSIBA WA RAIS MSTAAFU MZEE BENJAMINI WILLIAM MKAPA



Waombolezaji wakiwa kwenye mstari wakisubiri kutoa heshima zao za mwisho kwa mwili wa Rais mstaafu, Benjamin Mkapa, kwenye uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, jana.



Kibanda kilichotumika kuagwa kwa mwili wa Rais mstaafu Benjamin Mkapa, katika uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.



Maofisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wakiwa wamebeba mwili wa Rais mstaafu, Benjamin Mkapa, wakiupeleka sehemu ya kuuagia, jana.



Mjane wa Rais mstaafu, Benjamin Mkapa, Mama Anna Mkapa, akiingia na familia yake katika uwanja wa Uhuru.



JenezalililobebamwiliwaRaismstaafu Benjamin Mkapa, likimwagiwa maji ya baraka wakati wa Ibada ya Misa katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA ZOTE: ANTHONY SIYAME**



Maandamano ya Maaskofu wa Kanisa katoliki wakiingia kuongoza Ibada ya Misa ya kumuombea Rais mstaafu, Benjamin Mkapa.

# MSIBA WA RAIS MSTAAFU MZEE BENJAMINI WILLIAM MKAPA



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakisubiri kutoa heshima zao za mwisho kwa mwili wa Rais mstaafu, Benjamin Mkapa.



Baadhi ya mawaziri na wabunge wakisubiri kutoa heshima zao za mwisho kwa mwili wa Rais huyo mstaafu.



Waombolezaji wakiwa katika mstari wa kwenda kutoa heshima zao za mwisho.



Mmoja wa waombolezaji akiwa amebebwa na wahudumu wa Chama cha Msalaba Mwekundu, baada ya kupoteza fahamu .



Msafara uliobeba mwili wa Rais mstaafu Benjamin Mkapa, ukiingia uwanja wa Uhuru kwa ajili ya kuagwa jijini Dar es Salaam, jana.



Gari lililobeba mwili wa Rais mstaafu, Benjamin Mkapa, likiingia Uwanja wa Uhuru kwa ajili ya Misa na kuagwa. **PICHA ZOTE: JUMANNE JUMA**

HABARI KITAIFA

# Vita dhidi ya utapiamlo yahimizwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imewahimiza Watanzania kupambana na utapiamlo, huku ikiwataka wazazi kuongeza kasi ya kuwanyonyesha watoto maziwa ya mama na ulishaji wa vyakula vya nyongeza.

Aidha, kutokana na tatizo la utapiamlo, inakusudia kuanza kutoa programu zinazojumuisha matunzo ya mtoto kwa familia pamoja na kwenye huduma za shule za awali, kwa kuwa imethibitika kuwa na ufanisi katika kupambana na tatizo la utapiamlo

Hayo yalisemwa na Ofisa Lishe, Mtafiti waTaasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) , Eliasaph Mwana , wakati akitoa mada kuhusu hali ya lishe nchini kwenye mafunzo kwa waandishi wa habari wa mkoa wa Morogoro yaliyotolewa na Taasisi hiyo.

Taasisi hiyo iliyoko chini ya Wizara hiyo, imekuwa ikiendesha mpango maalumu wa mafunzo kwa waandishi wa habari nchini kuhusu namna ya kuandika na kuripoti kwa ufasaha na usahihi habari za lishe .

Mwana alisema kuwa licha ya kuwa ni msingi wa uchumi, maendeleo na afya ya binadamu kwa sababu lishe bora ina mchango mkubwa katika kuboresha afya na ustawi wa jamii.

Alisema ni muhimu kuwekeza katika lishe ili kufikia uchumi wa kati ambao kwa sasa umefikiwa, na pia kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 na Malengo Endelevu ya Dunia 2030.

"Kuwekeza katika lishe huleta faida ambazo ni mara 10 hadi 40 zaidi ya kiwango kilichowekezwa, lishe ni muhimu kiuchumi kwa sababu huongeza kiwango cha uelewa na ufaulu katika elimu na uzalishaji mali," alisema Mwana.

Alkisema ni muhimu katika makuzi ya ubongo na uwekezaji kwa mtu.

Naye Ofisa Lishe mtafiti, Victoria Kariathi,alisema afua za lishe zina faida kubwa ukilinganisha na gharama ukuaji na maendeleo duni ya ubongo kwa watoto huathiri uelimikaji wa watoto, hivyo kuathiri uwezo wa kujifunza na kuelimika.

Akizungumzia utapiamlo, alisema kuwa unasababisha udumavu, upungufu wa damu, upungufu wa kinga mwilini, uzito uliokithiri, kisukari, kansa, magonjwa ya moyo na kuathiri ukuaji na uzalishaji katika Taifa.



Wajumbe wa bodi ya maji ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Shinyanga (SHUWASA), wakiwa katika ziara ya kutembelea mradi wa uzalishaji maji kutoka Ziwa Victoria na kuyapeleka mkoani Shinyanga, katika Kijiji cha Ihelele wilayani Misungwi mkoani Mwanza, ambao ulijegwa mwaka 2003 na Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa, **PICHA:MARCO MADUHU**

# Pwani wapewa angalizo magonjwa ya mlipuko

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WANANCHI mkoani Pwani wametakiwa kuzingatia kanuni za usafi ili kuepuka kupata magonjwa ya mlipuko.

Kwa sasa mkoa wa Pwani unaendesha kampeni ya kuhamasisha jamii kujikinga na magonjwa mbalimbali itakayofanyika kwa siku 30 katika halmashauri zote.

Akizungumza uzi mjini Kibaha wakati wa muendelezo wa kampeni hiyo ambayo ilifanyikia katika soko la Loliondo mjini Kibaha, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Gunini Kamba, alisema kampeni hiyo inaratibiwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na wadau ambao ni Chama Cha Msalaba Mwekundu.

Alisema, wananchi wanatakiwa kuchukua tahadhari za magonjwa ya mlipuko ukiwamo usafi wa mazingira na kuweka maji ya kunawa mikono katika maeneo mbalimbali ya huduma.

Alisema, kampeni hiyo inakwenda sambamba na msisitizo wa kupeleka watoto walio chini ya miaka mitano kliniki pamoja na kuhamasisha wananchi kuwa na bima za afya ambazo zitawasaidia kupatiwa matibabu wakiugua ghafla hata wakiwa hawana fedha.

Ofisa kutoka kitengo Cha Elimu ya Afya kwa Umma cha Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Orsolina Tolage, alisema kampeni hiyo inafanyika katika maeneo mbalimbali nchini.

Tolage alisema katika kampeni hiyo, waratibu ngazi ya Halmashauri watakuwa wanahamasisha pia wazazi na walezi kupeleka watoto wao kliniki kupata chanjo, kwani katika kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa corona wengi walisitisha kwenda kliniki.

Aidha, alisisitiza wananchi kuendelea kufuata kanuni na udhibiti wa afya kama ilivyo katika kipindi cha ugonjwa wa corona. Kampeni hiyo inafanyika katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu zikiwamo shuleni, makoko na stendi ili kuufikisha ujumbe kwa urahisi.

# Wadau wapigwa jeki kuchangia Ukimwi

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WADAU mbalimbali mkoani Mwanza wamekabidhiwa masanduku 10 kwa ajili ya kuchangia mfuko wa udhamini wa kudhibiti ugonjwa wa Ukimwi nchini.

Akizungumza wakati akimkabidhi masanduku hayo, Mkuu wa mkoa wa Mwanza, John Mongella, kwa ajili ya kuwakabidhi wadau hao, Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania ( TACAIDS),Dk.. Leonard Maboko, alisema mfuko huo ulianzishwa rasmi mwaka 2015 na hayati Rais mstaafu, Hayati Benjamini Mkapa.

" Tumeondokewa na mwanzilishi wa TACAIDS, lakini uwapo wetu leo hapa ni kutokana na maono yake, hivyo huu mfuko ni kwa ajili ya kuwahudumia Watanzania pia asilimia 25 ya fedha zinatumika kwa ajili ya kuzuia maambukizi mapya," alieleza Dk. Maboko.

Naye Mongella alisema anawaanini wadau hao kwani wanathibitisha wana nia na dhamira ya dhati katika kupambana na vita hiyo kwa kuwa katika maeneo yao wana sera ya kupambana na ugonjwa huo.

Aliongeza kuwa mapambano hayo yanahitaji ufadhili, lakini si wa kutoka nje kwa sababu ni hatari kwa mapambano, na kwamba pia utoaji wa elimu kutasaidia kuleta hali mpya.

" Huwezi kuwa unapambana na vita ukategemea msaada tu wa marafiki kwani misaada hiyo inaweza kuja ikiwa imeambatanishwa na ajenda zingine na kusababisha vita yao isifanikiwe sana... lakini kwenye hili zoezi mtu akiweka mia, mia mbili au tano kwetu ina maana sana kwa sababu hatukuamka asubuhi tukiwa nayo hiyo kaja kutuwekea," alisema Mongella

# Waishukuru jumuiya kuwajengea visima

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

IMEELEZWA kuwa kukosekana kwa stadi za maisha kwa wanafunzi, kumesababisha kuwa na jamii ya watu wasiojitambua.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki mjini Bagamoyo na Dk. Enock Mlyuka wakati akitoa mafunzo ya stadi za maisha kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Bagamoyo.

Dk. Mlyuka ambaye ni Mkurugenzi wa Taasisi ya kijamii isiyo ya kiserikali ambayo inahudumia jamii ya Tamcare, alisema stadi za maisha ni muhimu kwa vijana ili kuandaa taifa lililo bora na kuwa na raia raia wema wenye kujitambua.

"Wazazi wengi wanalipa ada kwa watoto wao ili wasome, lakini hawana muda wa kuwafuatilia na kuongea nao, yanayoendelea maishani yanatokana na makuzi, elimu inatakiwa kwenda sambamba na nidhamu kwa vijana," alisema Dk. Mlyuka.

Alisema, stadi za maisha zinawasaidia vijana kujitambua, kuwajibika na kuwa na maarifa ya kukabiliana na changamoto watakayokutana nayo kwenye maisha.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Bagamoyo, Khalfan Milongo, alishukuru Taasisi ya Tamcare kwa mafunzo hayo ambayo alieleza kuwa yamewakumbusha mambo muhimu, ikiwa ni pamoja na kuzingatia muda wakiwa shuleni.

## Jamii yaelekezwa fursa zaidi za utalii

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

JAMII mkoani Kagera imetakiwa kutambua fursa za utalii kwa kushiriki na kujifunza mambo mbalimbali yaliyomo ndani ya mkoa huo.

Utalii huo ambao umegawanyika sehemu mbalimbali ni fursa kwa jamii kutumia mambo yanayoonekana na yaliyotumiwa na mababu

Akizungumza na baadhi ya washiriki 10 na wasikilizaji wa kipindi cha utalii kupitia kipindi cha Redio ya Jamii (KCR) Manispaa ya Bukoba, Katibu Tawala wa mkoa huo, Prof. Faustine Kamuzora, alisema kuwa, kujifunza kwa kutalii kunajenga akili na ubongo kuchangamka.

Prof. Kamuzora alisema jamii ya mkoa wa Kagera in maeneo ya kujifunza endapo itapenda kushiriki na wadau wa utalii kupata mwongozo wa maeneo.

Alisema kuna maeneo ya enzi za mababu, ambayo walitumia kufua vyuma, maporomoko ya maji na mito inayosadikiwa kutibu magonjwa.

"Mkoa wetu una fursa nyingi, tuna hifadhi za Taifa Ibanda Kyerwa na Rumanyika Karagwe yaliyopewa hadhi, lakini bado kuna mambo ya vivutio vya asili maeneo mbalimbali,"alisema Prof. Kamuzora.

Kwa upande wake Naibu Mkurugenzi wa Redio hiyo, Joas Kaijage, alisema kuwa lengo la kuandaa kipindi cha utalii kwa jamii ni kuondoa hali ya mazoea na kuweka mtazamo mpya wa jamii juu ya hifadhi zinazopatikana mkoani hapa.

Alisema kama jamii ikiwa na uelewa mkubwa kupitia wasikilizaji 311, ambao waliweza kuchangia mada iliyoandaliwa, kuna uwezekano wa kupata mabadiliko na kuinua uchumi.

"Mtazamo wetu ni elimu, utambuzi wa hifadhi ili zitakapoanza waweze kutumia fursa ya kutembelea kujifunza na kufanya biashara kuinua uchumi wao," alisema Kaijage.

Mwenyekiti wa utalii mkoani Kagera, Mary Kalikawe, alisema kwa kipindi hiki ambacho mipaka ya nchi imefungwa kutokana ugonjwa wa COVID-19, ni muda wa kufanya utalii wa ndani.

# Waziri Mpango akoleza vita dhidi ya rushwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imesema imedhamiria kwa dhati kuondoa uzembe na vitendo vyovyote vya rushwa mahala pa kazi ikiwa ni pamoja na kubana matumizi yasiyo ya lazima ili kuongeza tija.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ndiye aliyebainisha hayo kwenye ufunguzi wa kikao cha kwanza cha Baraza Kuu la Nne la Wafanyakazi wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA).

Katika Hotuba yake iliyosomwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, alisema ni wajibu wa kila mfanyakazi wa Taasisi hiyo kuhakikisha anafahamu wajibu wake mahali pa kazi, anatekeleza malengo aliyopangiwa katika muda uliopangwa, kutunza mali na vitendea kazi pamoja na kuwahi kazini.

Dk. Mpango alisema nafasi waliyopewa ya kuwatumikia Watanzania kupitia taasisi hiyo ni dhamana na ni vyema wakafanya kazi kwa bidii ili kukidhi matarajio ya wananchi na falsafa ya serikali ya awamu ya tano ya 'hapa kazi tu'.

Hata hivyo pamoja na hayo, Serikali itaendelea kujali na kuzingatia utaratibu uliopo wa kuwa na mabaraza ya wafanyakazi kwa kila taasisi kwa kuwa mabaraza hayo ni kiunganishi muhimu kati ya menejimenti na wafanyakazi ndani ya Taasisi za Serikali.

Alisema lengo la Serikali katika Taasisi zake ni kutaka kuleta mafanikio katika nyanja zote zinazofanywa na wafanyakazi wake na ili kufikia mafanikio chanya, ni lazima kuwa na uhusiano mazuri kati ya waajiri na waajiriwa pamoja na kuwashirikisha wafanyakazi mambo muhimu yanayofanywa na Taasisi husika.

Dk. Mpango alisema bila ushirikiano kati ya mwajiri na mtumishi ni vigumu Taasisi kutimiza malengo yake, kwani Serikali bado inaamini kuwa Mabaraza ni kiungo muhimu katika kuleta mafanikio hayo, huku akisema mabaraza hayo yapo kwa mujibu wa sheria.

Dk. Mpango aliipongeza TIA kwa mafanikio makubwa waliyofikia katika kutoa elimu yenye ubora, ambayo imechangia kupata wataalamu wanaochangia katika ujenzi wa Taifa la Tanzania.

Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa TIA, Prof. Carolyne Nombo, alisema utafiti unaofanywa na TIA kwenye baadhi ya halmashauri nchini una mchango katika ukusanyaji wa mapato kwa kuwezesha halmashauri hizo kuibua vyanzo vipya vya mapato na kubaini namna bora ya kudhibiti upotevu wa mapato kutokana na ukwepaji kodi na ushuru.

Alisema katika kikao hicho wajumbe wa Baraza hilo watakuwa na fursa ya kupitia maazimio ya kikao cha Baraza lililopita, kuangalia mafanikio na kuweka vipaumbela kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na kujadili changamoto zinazowakabili na kupata majibu ya changamoto hizo. Alisema hadi sasa taasisi ina jumla ya wanafunzi 18,717 katika kampasi zote sita nchini zilizopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Singida, Mwanza, Kigoma na Mtwara.




Meneja wa Kituo cha Mawasiliano ya Wateja cha Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Lello Mmassy, akizungumza katika mkutano na wanahabari kuhusu mafanikio ya kituo hicho katika mwaka mmoja jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC ataka haki itendeke ugawaji vizimba

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, ameuagiza uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kuhakikisha ugawaji wa vizimba katika soko kuu la mkoa unafanyika kwa haki na utulivu ili kusiwapo na malalamiko.

Msulwa aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara wa soko la Manzese waliohama kupisha ujenzi wa soko kuu jipya mwaka juzi, ambapo aliitaka Manispaa kuaanda utaratibu mzuri wa kuwarudisha.

"Ujenzi wa soko kuu la mkoa wetu upo kwenye hatua za mwisho kukamilika, hivyo leo nauagiza uongozi wa Manispaa kuhakikika ugawaji wa vizimba katika soko hilo unafanyika kwa haki na kusiwapo malalamiko yoyote," alisema Msulwa.

Alisema mbali na ugawaji wa vizimba hivyo kufanyika kwa haki, lakini pia wafanyabiashara waliokuwapo awali na kukubali kupisha ujenzi bila kinyongo ni lazima wapewe kipaumbele cha kupatiwa vizimba na kisha wengine wafuate.

Mkuu huyo wa wilaya alisema serikali imetumia fedha nyingi kwenye ujenzi wa soko hilo, na kwamba itakuwa ni aibu kubwa endapo zoezi la ujawaji wa vizimba litatawaliwa na vurugu na fujo, hivyo aliwatoa hofu wafanyabiashara wote.

Msulwa alisema kuwa kabla wafanyabiashara kuruhusiwa kurudi sokoni hapo watatengenezewa namba zao ili kuonyesha maeneo watakayokaa katika vizimba vyao lengo likiwa ni kuepusha fujo na viashiria vya uonevu.

"Nasikia kuwa kuna utaratibu umeandaliwa wa kuwaruhusu wafanyabiashara kuingia katika soko hili... hakikisheni zoezi hili linafanyika kwa mpangilio mzuri na kusiwapo na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara hawa," alisema Msulwa.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara wote watakaopata fursa ya kufanya biashara zao katika soko hilo kulithamini soko hilo kwa ujumla na kulinda miundombinu yake, na kwamba serikali haitamfumbia macho atakayefanya uharibifu wa aina yoyote.

Alisema imani yake ni kuwa uchumi wa wafanyabiashara wa Mkoa wa Morogoro kupitia soko hilo utaimalika, hivyo kuiwezesha Halmashauri ya Manspaa na mkoa kwa ujumla kuwa na mapato mengi yatakayoleta tija kwa taifa.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Dk. Tito Kagize, alisema kuwa wamejipanga vizuri katika ugawaji wa vizimba, na kwamba zoezi zima la ugawaji vizimba utafanyika kwa haki bila upendeleo wa aina yoyote.

Dk alisema wafanyabiashara watakaopewa kipaumbele cha kufanya biashara katika soko hilo ni 764 wanaotokea soko la Mawenzi na Manzese Manispaa ya Morogoro ambao walisaini mkataba wa kupisha ujenzi wa soko jipya la mkoa.

Nao wafanyabiashara walipongeza serikali kwa uamuzi wa kujenga soko hilo, na kwamba watahakikisha ukusanyaji mapato unafanyika kwa uaminifu kwa maslahi ya Morogoro na taifa kwa ujumla.

Nipashe
Spotika



NYOTA 10 WALIOTAMBA EPL 2019-20 BILA MATARAJIO UK. 12&13



# WACHEZAJI BORA WA5 WALIOCHEZA NA MESSI

## ISIKUPITE

OLIVIER Giroud ameifungia timu hiyo ya taifa mabao 39 katika mechi 97. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 33 anahitaji mabao matatu tu kuweza kumpiku Michel Platini na kushika nafasi ya pili kama mfungaji bora wa wakati wote wa Ufaransa, nyuma ya Thierry Henry, aliyefunga mabao 51 kati ya mwaka 1997 na 2010.



**BARCELONA,** Hispania

IKIWA inachukuliwa kwamba, Lionel Messi ni mchezaji bora zaidi duniani na pengine katika historia ya mchezo wa soka, huku nahodha huyo wa Barcelona akiwa amecheza na nyota kadha bora kabisa katika karne ya 21.

Barcelona imeshuhudia mafanikio makubwa kwa kipindi cha muongo mmoja kwa kujitwalia mataji kadhaa na kwa kiasi kikubwa mafanikio hayo yamebebwa mabegani mwa Messi na wachezaji wenzake.

Messi ametengeneza uhusiano mzuri zaidi na wachezaji kadhaa ndani ya uwanja. Hii ni orodha ya wachezaji bora watano aliocheza nao Messi dimbani.

Heshima kuwataja: Neymar, Carles Puyol, Gerard Pique, David Villa na Deco

5. Dani Alves

Popote pale, Dani Alves mara zote anamtaja Messi kama mchezaji bora zaidi dimbani aliyewahi kumshuhudia.

Alves alijiunga na Barcelona mwaka 2008 na kuwa mmoja wa usajili uliofanikiwa zaidi chini ya kocha, Pep Guardiola. Nyota huyu wa Brazil alikuwa akishirikiana vizuri zaidi na Messi ambaye alikuwa akicheza kama winga wa kushoto.

Alves ameshinda mataji matatu ya Ligi ya mabingwa Ulaya akiwa na Barcelona na alikuwa akimlisha sana mipira Messi zaidi ya mara 42.

### 4. RONALDINHO

Huyu ndiye anatajwa kama alikuwa na mchango mkubwa zaidi kukua kikosi kwa Messi. Ronaldinho kama ilivyo kwa Messi leo, raia huyo wa Brazil alikuwa na uwezo wa kusepa na kijiji cha walinzi.

Ronaldinho alikaa Barcelona hadi mwaka 2008 na ndio alikuwa mwalimu wa Messi klabuni hapo.

Raia huyu wa Brazil, Ronaldinho ndio alimtengenezea Messi bao lake la kwanza akiwa na jezi ya Barcelona na tangu hapo La Pulga huyo hajawahi kushuka tena. Ronaldinho pia ni mchezaji pekee wa Barcelona kupewa heshima ya kusimama na kupigiwa makofi na mashabiki wa Real Madrid pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

### 3. LUIS SUAREZ

Luis Suarez kwa uhakika kabisa ndiye anayevutiwa zaidi na Messi pale Barcelona. Pamoja na urafiki wake na Messi, raia huyu wa Uruguay anafurahia maisha ya soka uwanjani akicheza na nyota huyo wa Argentina.

Suarez alikuwa kwenye kiwango cha juu pale Barcelona na alishinda taji la Ligi ya mabingwa Ulaya katika msimu wake wa kwanza klabuni hapo. Straika huyo wa zamani wa Liverpool alikuwa na upatina mzuri zaidi na Messi na Neymar chini ya kocha Luis Enrique. Watatu hao kwa pamoja walifunga jumla ya mabao 122 katika msimu wa 2014-15.

Na mshambuliaji huyo alifunga mabao 40 katika msimu uliofuata kule LaLiga na kuwa mchezaji wa kwanza nje ya Messi na Cristiano Ronaldo kutwaa tuzo ya Pichichi kwa kuwa mfungaji bora tangu mwaka 2009.

### 2. XAVI

Kwa sasa majukumu yote ya Barcelona yanabebwa na Messi. Lakini ukirudi nyuma miaka michache iliyopita Messi hakuwa na mzigo huo, kwani majukumu yalikuwa chini ya Xavi Hernandez.

Xavi alikuwa 'mchawi' katika nafasi ya kiungo wa kati. Kiungo huyo wa kimataifa wa Hispania alikuwa nguzo muhimu zaidi kwa kikosi cha Barcelona katika kutengeneza mashambulizi.

Xavi pengine ni mmoja wa wachezaji wenye akili zaidi ambaye Messi alicheza naye.

### 1. ANDRES INIESTA

Andres Iniesta pengine atabakia kuwa mchezaji bora zaidi ambaye Messi amewahi kucheza nae. Iniesta ndio mchezaji pekee uwanjani ambaye anaweza kuwa kwenye daraja moja na Messi.

Iniesta alikuwa ndio injini ya Barcelona pale kwenye kiungo ya kati, huku akishirikiana kwa karibu na Xavi na Messi.

Iniesta alimwaga machozi wakati akiagwa pale Barcelona mwaka 2018 na aliondoka akiwa na mataji manne ya Ligi ya mabingwa Ulaya na 9 ya LaLiga.

Extra Time

# NYOTA 10 WALIOTAMBA EPL 2019-20 BILA MATARAJIO



DANNY INGS

**LONDON,** England

MSIMU wa Ligi Kuu ya England 2019-20 hautasahaulika katika zama za soka la kisasa. Mlipuko wa virusi vya corona Ulaya ulisababisha kusimamishwa kwa shughuli zote za soka barani humo na ilikuwa ni mara ya kwanza tangu vita ya pili ya dunia.

**Hata hivyo, baada ya miezi mitatu Ligi Kuu ya England ikarudi tena na kuendelea.**

Liverpool ndio mkubwa wa ligi hiyo baada ya kutawala kwa msimu wote na wamelitwaa taji hilo kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 30. Kikosi hicho cha Jurgen Klopp kilishinda taji la Ligi Kuu huku zikiwa zimebaki mechi saba.

Kama ilivyo kwa ligi nyingine yoyote, wachezaji kadhaa wameongeza heshima zao kwa kuonesha kiwango cha juu, huku majina mengine yakishindwa kutamba.

Makala hii inakuchambulia wachezaji 10 wa Ligi Kuu ya England ambao wamefanya makubwa tofauti na matarajio ya wengi msimu huu.

### #10 DOMINIC CALVERT-LEWIN | EVERTON

Mshambuliaji huyu wa Everton, Dominic Calvert-Lewin hatimaye amekuwa na msimu wa kuvutia, ikiwa ni miaka minne tangu kutua kwenye Ligi Kuu ya England. Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 23 amekuwa nguzo muhimu mno kwa kocha Carlo Ancelotti baada ya kutua pale Goodison Park.

Tangu kuchaguliwa kwa Muitaliano huyo Desema mwaka 2019, Calvert-Lewin alifunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho kweye ligi kuu, ikiwamo mabao muhimu dhidi ya Manchester United na Arsenal.

Mcheza huyu wa zamani wa Sheffield United amekuwa mmoja wa wachezaji walioimarika zaidi katika msimu huu na ana mengi yanakuja kutoka kwake.

### #9 MASON MOUNT | CHELSEA

Mason Mount alifanya makubwa wakati akicheza kwa mkopo kule Derby County msimu uliopita, ambapo aling'aa chini ya Frank Lampard. Mwaka mmoja baadae wawili hao wakaungana tena pale Stamford Bridge.

Akiwa amechukua mikoba ya kuinoa Chelsea, Lampard aliendelea kumtumia Mount kama mmoja wa wachezaji wake muhimu vijana. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, alifunga mabao sita katika mwanzo wake wa kwanza kwenye ligi kuu ya England.

Mount amecheza karibia katika mechi zote za Ligi Kuu na kuwa mmoja wa nguzo muhimu kwa kikosi cha Lampard.

### #8 DEAN HENDERSON | SHEFFIELD UNITED

Sheffield United imewashangaza wengi kwenye ligi kuu msimu huu, na shukrani kubwa ni kwa Dean Henderson. Golikipa huyu kijana ambaye anacheza kwa mkopo hapo akitokea Manchester United, amefurahia msimu wake wa kwanza kwenye ligi kwakuwa na kiwango cha kuvutia.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23 kwa sasa anatajwa kama ndiye mrithi wa David de Gea ambaye ameonekana kufanya makosa mengi kwa mashetani wekundu.

Kocha wa England, Gareth Southgate anaweza baadae kumuita kipa huyo kwenye kikosi chake ili akatoe ushindani dhidi ya Jordan Pickford.

### #7 JACK GREALISH | ASTON VILLA

Mengi yamezungumzwa kuhusu Jack Grealish baada ya msimu wake wa kwanza wa Ligi Kuu ya England akiwa na Aston Villa, wakitoka ligi daraja la kwanza ambapo walishuka msimu wa 2015-16.

Grealish mwenye umri wa miaka 24 amekuwa na mchango mkubwa kwa kikosi hicho hasa katika safu ya kiungo.

Grealish amekuwa mmoja wa viungo bora zaidi katika Ligi Kuu ya England msimu huu na kwa vyovyote usajili wa kwenda timu nyingine unaweza kugharimu fedha nyingi.

#6 Phil Foden | Manchester City

Amesifiwa kama mchezaji kijana anayekuja juu na kocha wake, Pep Guardiola na Phil Foden ameendelea kuimarika msimu huu na kujikuta akipata nafasi ya kucheza mara kwa mara katika kikosi cha Manchester City.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 20 tayari ameshinda mara mbili taji la Ligi Kuu ya England na anatazamiwa kuwa mrithi wa David Silva ambaye anaondoka kipindi hiki cha majira ya joto. Muingereza huyu amecheza mechi 35 katika mashindano yote na katika mechi 21 za Ligi Kuu, amefunga mabao saba na kutoa pasi za mwisho tisa.

### #5 ADAMA TRAORE | WOLVES

Adama Traore ni mmoja wa wachezaji wanaovutia zaidi katika soka la sasa duniani. Winga huyo amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi msimu huu.

Winga huyu wa zamani wa Barcelona amekuwa msaada mkubwa kwa kikosi cha Wolves na amekuwa akitolewa macho na timu nyingi barani Ulaya. Katika umri wake wa miaka 24 amekuwa akicheza kwa upatina mzuri na Raul Jimenez pale Wolves.

Amefunga mabao sita na pasi za mwisho 12 kwenye mashindano yote na Traore anatabiriwa kuwa atakuwa na mafanikio makubwa zaidi kwa siku za usoni.

### #4 BUKAYO SAKA | ARSENAL

Alikuwa hajulikani kabla ya msimu huu, lakini haraka, Bukayo Saka amejijengea jina lake kama mmoja wa vijana wenye vipaji vya ukweli pale Arsenal. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 alianza kucheza kwa mara ya kwanza chini ya kocha, Unai Emery lakini amekuwa mchezaji muhimu chini ya Mikel Arteta, huku akiendelea kujifunza na kukua zaidi.

Kiasili huyu ni winga wa kushoto, lakini kutokana na majeruhi yaliyoiandama Arsenal amekuwa akicheza kama kiungo mshambuliaji.

Muingereza huyu amecheza mechi 38 katika mashindano yote kwa Arsenal, akifunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho 11 kwa jina lake.

Saka hivi karibuni alisaini mkataba wa muda mrefu na washikabunduki hao na inaonekana atakuwa muhimu zaidi kwa kikosi hicho cha Arteta kwa miaka inayokuja.

### #3 MASON GREENWOOD | MANCHESTER UNITED

Kuchomoza kwa Mason Greenwood imekuwa moja ya habari kubwa msimu huu, kinda huyu ameendelea kuwa na mchango mkubwa kwa kikosi cha Manchester United.

Akiwa ameanza msimu huu kwa kujifunza kutoka kwa wachezaji kama Marcus Rashford na Anthony Martial, nyota huyu mwenye umri wa miaka 18 na amejiimarisha yeye mwenyewe na kuwa na nafasi katika kikosi cha kwanza.

Greenwood amefunga mabao 18 na kutoa pasi za mwisho tano katika mechi 45 alizocheza kwenye mashindano yote pale Manchester United.

### #2 DANNY INGS | SOUTHAMPTON

Baada ya kusumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara, Danny Ings hatimaye ameonesha kiwango chake kwenye ligi Kuu, Muingereza huyu kwa sasa anafurahia msimu bora zaidi kwake.

Ings alitua hapo kwa mkopo akitokea Liverpool kabla ya kusaini mkataba wa kudumu kipindi cha majira ya joto kilichopita. Katika umri wake wa miaka 27, nyota huyu wa zamani wa Burnley amefunga mabao 20 kwenye ligi kuu msimu huu.

### #1 JORDAN HENDERSON | LIVERPOOL

Huyu ni nahodha wa Liverpool, Jordan Henderson awali alikuwa akishutumiwa zaidi na mashabiki kwa kiwango chake hasa kutokana na kubeba jukumu kubwa lililokuwa chini ya gwiji, Steven Gerrard.

Hata hivyo, Henderson amekuwa na kiwango cha kuvutia sana na kuwa mmoja wa wachezaji bora wa Liverpool kwa misimu miwili mfululizo.

Katika umri wake wa miaka 30 amekuwa na mchango mkubwa kwa Liverpool katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi pamoja na ligi ya mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Henderson nyota wa zamani wa Sunderland amekuwa akiaminiwa sana na kocha, Jurgen Klopp.

## Nukuu


"Musti ameumia, bado hatujajua atakuwa nje kwa muda gani, lakini katika mechi zetu zijazo hatakuwapo," amesema Arteta akiwaambia waandishi wa habari."Nina shaka kama atakuwa fiti kwenye fainali, tutaangalia kwa siku zinazokuja. Lakini kwa wakati huu sina uhakika kama atakuwepo." **Kocha wa Arsenal Mikale Ateta akielezea hali ya Shkodran Mustafi**



"Sina malalamiko, lakini nimeumizwa. Sasa ni wakati wa kurudi kwa Unai Emery na natumaini kuwapeleka juu kadili itakavyowezekana." **Unai Emery mara baada ya kuteuliwa kuwa kocha mpya wa ya Villarreal.**



"Nafikiri mara zote Ujerumani ina wachezaji wazuri zaidi vijana, hakuna swali kuhusu hilo. Sijui kwanini (klabu) zinawaangalia sana wachezaji wetu vijana." **Winga wa Bayern Munich, Leroy Sane.**






Wachezaji na baadhi ya viongozi wa Simba wakisherehekea ubingwa kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini Mtwara baada ya kumamilika mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Ndanda na kutwaa Ubingwa wa msimu wa 2019/20, ikiwa pia ni kwa mara ya tatu mfululizo. **PICHA: MAKTABA**

# SIMBA ILIPOISHINDWA REKODI YAKE YENYEWE

**Na Adam Fungamwango**

MASHABIKI wa Simba wamekuwa na furaha kubwa baada ya timu yao kutwaa ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo, msimu huu wa 2019/20, msimu uliopita wa 2018/19 na msimu wa 2017/18.

**Hata hivyo, timu hiyo imeshindwa kuifikia rekodi yake yenyewe ya pointi za msimu uliopita. Kabla ya mechi yake ya jana dhidi ya Polisi Tanzania, tayari ilikuwa na pointi 85, ambazo hata kama ikishinda itafikisha pointi 88 tu ambazo haziwezi kuzifikia pointi za msimu uliopita.**

Pamoja na hayo, pointi hizo zimevunja rekodi za msimu wa 2017/18, huku zikishika nafasi ya pili kwa pointi nyingi kuzipata Simba tangu mfumo mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara ubadilike kuanzia msimu wa 2007/08.

Tangu mfumo huo uanze, Simba imepata ubingwa mara tano na rekodi zinaonyesha kuwa msimu uliopita ndiyo Simba ilivunja rekodi ya kuzoa pointi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mwandishi wa makala haya amekusanya pointi zote ambazo Simba imezipata kwenye msimu ya ubingwa wake tangu mfumo huo uanze tukianzia na msimu uliopita.

**UBINGWA WA 2018/19 (POINTI 93)**

Hii ilikuwa ni msimu uliopita ambao ndiyo msimu bora zaidi kwa Simba kwenye ubingwa wake wote mara tano tangu ilipoanza kuchukua msimu wa 2009/10, mfumo mpya wa Ligi Kuu ilipoanza.

Ilikusanya jumla ya pointi 93 ambazo hata kama mechi ya mwisho dhidi ya Polisi Tanzania ikishinda basi itafikisha pointi 88 tu ambazo ziwezi kabisa kuzifikia hizo.

Msimu huu Simba ilicheza mechi 38, ikashinda mechi 29, sare sita, ikafungwa mechi tatu tu, ikifunga magoli 77 na kufungwa magoli 15, ikizoa pointi hizo.

Ukiangalia takwimu ni kwamba hata idadi ya mechi za kufunga, msimu huu kama Simba ikishinda mechi yake dhidi ya Polisi Tanzania jana basi itafikisha mechi 27 tu za kushinda ambazo pia hazijaweza kuifikia rekodi ya msimu uliopita, na itakuwa ni pungufu ya mechi mbili kama itakuwa imeshinda.

Msimu uliopita, Simba ilipoteza mechi tatu tu, lakini tayari msimu huu kabla ya mechi ya jana ilikuwa imepoteza mechi nne.

Hata sare, msimu huu imetoa sare saba kabla ya mechi ya mwisho, huku msimu ulipita ikitoa sare sita tu.

**UBINGWA WA 2017/18 (POINTI 69)**

Msimu wa 2017/18, Simba ilitwaa ubingwa ikiwa imekusanya pointi 69. Ukiangalia pointi hizi ni chache zaidi kuliko za msimu huu, kwani kabla ya mechi ya mwisho wa jana, tayari ilikuwa na pointi 85.

Msimu huo, Simba ilicheza mechi 30, ikishinda mechi 20, sare tisa, lakini iliweka rekodi ya aina yake kwa kupoteza mechi moja tu, ikifunga magoli 62, kufungwa magoli 15.

Huu ulikuwa ni ubingwa wa kwanza wa timu hiyo baada ya misimu mitano kupita.

**UBINGWA WA 2011/12 (POINTI 62)**

Simba ilitwaa ubingwa msimu wa 2011/12 ikiwa na pointi 62 tu ambazo zilikuwa chache zaidi kuliko misimu iliyofuata.

Ilicheza mechi 26, ikishinda mechi 19 ambazo nazo ni chache zaidi kuliko hata msimu wa 2017/18, ikitoa sare tano na kupoteza mechi mbili tu. na huu ndiyo uliokuwa msimu wa mwisho wa timu hiyo kutwaa ubingwa mpaka msimu mingine mitano iliyofuata, yaani 2017/18.

**UBINGWA WA 2009/10 (POINTI 62)**

Ni idadi hiyo hiyo ya pointi 62 ambayo ilipata baada ya msimu mmoja baadaye yaani 2011/12.

Huu ulikuwa ni msimu maalum kwa Simba kwani ilimaliza msimu bila kupoteza hata mechi moja.

Ni rekodi ambayo haijawekwa si na timu yoyote ile kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, bali hata Simba yenyewe haijairudia tena.

Ilicheza mechi 22, ikishinda mechi 20, sare mbili tu na ikacheza msimu mzima bila kupoteza, wakati huo ikiwa chini ya kocha Mzambia, Patrick Phiri.

**JE, WAJUA?**



NAHODHA wa Barcelona, Lionel Messi, ameitaka klabu yake kumchukua Marcelo Bielsa kutoka Leeds United na kumpa nafasi ya kuwa kocha mpya wa Barcelona, achukue mikoba ya Quique Setien wa sasa.



# 30,000 waondolewa daftari la wapigakura

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imewaondoa wapigakura 30,487 kwenye daftari la kudumu la wapiga kura kutokana na kukosa sifa kwa mujibu wa sheria.

Aidha, imekamilisha uteuzi wa watendaji watakaosimamia na kuendesha shughuli za uchaguzi katika majimbo ya Jamhuri ya Muungano na kata za Tanzania bara.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki jijini hapa na Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji wa Rufani mstaafu, Semistocles Kaijage, katika ufunguzi wa kikao kazi cha wasimamizi wa uchaguzi.

Alisema baada ya kutoa wapigakura ambao taarifa zao zimejirudia taarifa za awali zimeonesha kuwa daftari lina jumla ya wapigakura takribani milioni 29.

Alifafanua kuwa Tume hiyo imekamilisha uboreshaji wa daftari hilo ambao ulifanyika mara mbili kama ilivyoelekezwa katika Kifungu cha 15(5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 21(5) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

"Awamu ya kwanza ilianza Julai 18, mwaka 2019 na kukamilika Februari 23, mwaka 2020 kwa nchi nzima na awamu ya pili ilikuwa Aprili 17, mwaka 2020 na kukamilika Mei 4, mwaka 2020 na awamu ya pili ya uboreshaji ilifanyika sambamba na uwekaji wazi daftari la awali kwa awamu ya kwanza katika vituo 37,814 vilivyotumika katika uboreshaji wa awamu ya kwanza," alisema.

Alieleza kuwa Tume iliweka wazi uboreshaji wa awamu ya pili Juni 17-20, mwaka huu na kwamba katika uboreshaji wote wa awamu mbili wapiga kura wapya ni 7,326,552 walioandikishwa sawa na asilimia 31.63 ya wapiga kura 23,161,440 walioandikishwa mwaka 2015.

Aidha, alisema wapiga kura 3,548,846 waliboresha taarifa zao na wapigakura 30,487 waliondolewa kwenye daftari hilo.

Akizungumzia kuhusu uteuzi wa watendaji, Mwenyekiti huyo alisema watendaji walioteuliwa ni waratibu wa uchaguzi 28, wasimamizi wa uchaguzi 194, wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo 742 na wasimamizi wasaidizi ngazi ya kata 7,912.

"Tume inatambua kuwa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi watafanya kazi chini ya usimamizi wenu, hivyo mnatakiwa kuhakikisha mnawapangia majukumu watendaji hao ili kuwe na ufanisi katika zoezi la uchaguzi,"alisema.

Hata hivyo, alisema Tume inaendelea na mchakato wa ununuzi wa vifaa mbalimbali vya uchaguzi mkuu mwaka huu sambamba na uchapishaji wa fomu, sheria za uchaguzi, kanuni na maelekezo.

Kadhalika, alisema Tume imetoa vibali kwa asasi za kiraia 97 kwa ajili ya kutazama uchaguzi mkuu mwaka huu, pia imetoa vibali kwa asasi za kiraia 245 Tanzania bara na asasi za kiraia saba kutoka Tanzania Bara kwa ajili ya kutoa elimu kwa wapigakura wakati wa uchaguzi huo.



Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Wafanyabiashara soko la Sabasaba jijini Dodoma, Emmanuel Mtenga (wa pili kushoto), akiwa na wanachama alipokuwa akizungumza na wanahabari (hawapo pichani) kwenye utambulisho uliofanyika juzi .**PICHA PETER MKWAVILA.**

# Mwongozo wa corona watolewa kwa watalii

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imeainisha hospitali za kuchukua sampuli za kupima virusi vya ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na virusi vya corona kwa watalii na wanaosafiri nje ya nchi kwenye mikoa 10 nchini.

Mikoa yenye hospitali hizo ni pamoja na Mkoa wa Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Dodoma, Mara, Morogoro, Iringa na Kigoma.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Mabula Mchembe, Wizara hiyo imetoa mwongozo wa upimaji wa COVID-19 kwa watalii na wanaosafiri nje ya nchi.

Alisema serikali imeandaa mwongozo huo ili kuwapima COVID-19 watalii na wasafiri wanaoondoka nchini kuhakikisha wanakidhi matakwa ya usalama wa kimataifa. "Mwongozo huu kwa watalii unalenga kuweka utaratibu wa upimaji wa hiari kwa watalii wanaokwenda kwenye nchi ambazo zinahitaji wawe wamepima angalau saa 72 kabla ya safari zao na kuthibitishwa kama wako 'Negative," alisema.

Alisem gharama ya kipimo cha COVID-19 kwa Mtalii mmoja ni Dola za Marekani 50 na malipo yatafanyika kwa kufuata utaratibu wa malipo ya serikali.

"Mwongozo huu unaweka utaratibu wa maombi, upimaji, namna ya kupata majibu, uhakiki, mipakani, viwanja vya ndege na gharama za upimaji kwa watalii wanaoondoka, mwongozo huu pia unawataka watalii wanaoingia nchini kuwa na vyeti vya uthibitisho wa kutokuwa na maambukizi ya COVID-19 ili nchi ijiridhishe juu ya afya yao wanapoingia nchini," alisema.

Julai 20, mwaka huu, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alitoa mwongozo wa upimaji wa COVID-19 kwa watu wanaosafiri nje ya nchi ambapo gharama za upimaji kwa Raia wa Tanzania ni Sh.40,000, Raia mkaazi wa Tanzania Sh.60,000 na Raia wa kigeni ni Dola za Marekani 100.

# TAG yataka uchaguzi mkuu 2020 kuombewa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG), Dk. Barnabas Mtokambali amewataka Watanzania kuombea uchaguzi mkuu ili chama chochote cha siasa kisitumike kama kichaka cha maadui wasioipenda Tanzania.

Kauli hiyo aliitoa Jumamosi alipokuwa akizungumza na washiriki waliohudhuria ibada maalum ya kuweka wakfu Kanisa la TAG CANA lililopo Ilazo, Jijini Dodoma na uwekaji wa jiwe la msingi la kituo cha watoto cha kanisa hilo.

"Kila nchi ina maadui wake na hasa nchi yenye utajiri mwingi kama yetu, wao hutumia muda kama huu wa uchaguzi ili kupenyeza mabaya yao. Kwa hiyo, uchaguzi unaweza kulijenga Taifa au kulibomoa, na sisi tukiomba Taifa letu haliwezi kubomoka," alisema.

Alisema mwaka huu kuna uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani, Kanisa hilo lina wajibu wa kufanya maombi ufanyike kwa amani kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Aliwataka waumini wa kanisa kila kuiombea Tume ya Taifa ya Uchaguzi(NEC) ili izingatie na kuombea vyama vya siasa kwa kuwa maadui wengi hujipenyeza kupitia huko.

"Watanzania wote wamuombe Mungu ili viongozi wanaochaguliwa wawe ni chaguo la Bwana. Tumuombe Mungu ili tupate viongozi bora, siyo bora viongozi tena wanaotoka kwa Bwana," alisema.

Aliwasihi Watanzania kudumisha amani na utulivu kwa kuwa ni tunu za Taifa.

"Amani na utulivu ndiyo tunu yetu. Wana-TAG na Watanzania wote tusikubali kutumika kuvuruga amani, tusikubali kushiriki jambo lolote litakaloondoa amani ili tuvuke tukiwa na umoja na mshikamano," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Askofu Mkuu Dk. Mtokambali alisema kanisa hilo linapanga kuhamia Dodoma ili kupunguza gharama za uendeshaji kutokana na shughuli nyingi kufanyika Dodoma.

"Japo makao makuu ya TAG yako Dar es Salaam, kazi nyingi zinafanyika hapa Dodoma, inatugharimu sana kuja na kurudi kuonana na viongozi wa Serikali,tumefanya uamuzi wa haraka ili ifikapo Septemba mwakani, tuwe tayari tuko Dodoma," alisema.

Akizungumza katika hafla hiyo, Naibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Anthony Mavunde, aliwaomba waumini wamuombee Rais Dk. John Magufuli kwa kuipa heshima kubwa Dodoma.

"Ukiondoa Afrika Kusini, Dodoma imepata barabara ya mzunguko ya kilometa 112.3 yenye njia nne ambayo ikikamilika itaondoa msongamano katikati ya jiji, Tumepata soko kubwa la kisasa la Job Ndugai, tuna stendi ya kisasa yenye uwezo wa kuingiza magari 600, Tunasubiri uwanja wa mpira wa kisasa, uwanja wa ndege wa Msalato ambao barabara yake itakuwa na urefu wa kilometa tatu, ndefu kuliko viwanja vyote nchini," alisema.

Awali, akisoma risala kuhusu ujenzi wa kanisa na kituo cha watoto, Mchungaji Kiongozi wa kanisa hilo, Dk. Joel Hamuli, alisema ujenzi wa kanisa hilo ambao ulianza Aprili 16, 2018 na kukamilika Juni 2019, umegharimu Sh. milioni 98.





## Wanasiasa: kifo cha Mkapa ni pigo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wanasiasa mkoani Mbeya wamesema kifo cha aliyekuwa Rais wa awamu ya tatu, Hayati Benjamin Mkapa ni pigo kwa taifa, kwa maelezo kuwa alikuwa bado anahitajika kwenye maendeleo ya taifa na kwamba ni kifo cha kushtua.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ni miongoni mwa wanasiasa hao ambapo alisema kiongozi huyo ni miongoni mwa waliofanikiwa kuimarisha uchumi wa taifa kwa kuwahimiza Watanzania kufanya kazi kwa bidii.

Alisema Hayati Mkapa alikuwa kiongozi aliyekuwa anaamini katika ukweli na uwazi na hivyo alikuwa anawaambia Watanzania mambo ambayo yalikuwa yanawasaidia kuimarisha uchumi.

"Kwenye kitabu chake kijulikanacho kwa jina la 'My Life, My Purpose (Maisha Yangu, Kusudio Langu)' ameandika mambo mengi ambayo sasa yanabaki kama wosia kwetu, ameandika mambo mengi ambayo ukiyasoma yanasaidia kujua vitu vingi sana, tumuenzi kwa kufanya kazi kwa bidii," alisema Chalamila.

Alisema kiongozi huyo alikuwa mwadilifu, na kwamba alikuwa anakiri makosa anapobaini kuwa kuna uamuzi alikosea na kuongeza kuwa hata kwenye kitabu chake alieleza baadhi ya mambo hayo.

Naye Charles Mwakipesile, miongoni mwa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, alisema kifo cha rais Mstaafu Mkapa kimekuwa cha ghafla mno na kimewashtua Watanzania.

Alisema kiongozi huyo alikuwa miongoni mwa marais wastaafu, ambao wamekuwa msaada mkubwa katika CCM kwa kutoa ushauri wa namna ya kukiendesha chama hicho.

# 'Kupungua uhalifu kumepaisha uchumi'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imesema kadri matukio ya uhalifu yanavyopungua nchini ndivyo uchumi wa nchi unavyozidi kuimarika kwa sababu watu wanakuwa wanatumia muda mwingi kwenye uzalishaji mali, badala ya kutumia muda huo kukabiliana na uhalifu.

Hayo yalisemwa jijini Mbeya mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Prof. Sifuni Mchome, wakati wa mafunzo kwa maofisa wa Jeshi la Polisi na Magereza kutoka katika mikoa ya Mbeya na Iringa kuhusu utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa watoto walioko kwenye vituo vya polisi na magereza.

Alisema kupungua kwa matukio ya uhalifu kwenye nchi ni miongoni mwa vigezo vya kupima ukuaji wa uchumi wa taifa husika, hivyo akawataka maofisa wa majeshi hayo waliohudhuria mafunzo hayo kushughulikia makosa ya uharifu kwa kuzingatia sheria.

Alisema baadhi ya makosa ambayo yanafanywa na wananchi hasa wanyonge wakiwamo watoto sio lazima yakashughulikiwa kwa kufikishana magereza na kwenye vituo vya polisi na badala yake wayashughulikie kwa kusuluhisha na kupatanisha.

"Watu wakihudumiwa na kupewa msaada wa kisheria katika vituo vya polisi na magereza kwa wakati na haraka, tutaimarisha uchumi wetu wa kati kwa kuongeza uzalishaji, lakini pia tutawawezesha watoto wanaokinzana na sheria kuendelea na masomo," alisema Prof. Mchome.

Aliwataka maofisa hao waliohudhuria mafunzo hayo kuhakikisha wanawasaidia wenzao kuhakikisha wanazingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utoaji haki kwa watoto wanaokinzana na sheria.

Alisema kundi la watoto ni miongoni mwa makundi yanayotakiwa kupewa kipaombele wakati wa utoaji haki, na kwamba wanatakiwa kuhudumiwa kwa haraka ili kuepuka kuwakosesha haki zingine za msingi.

Mratibu wa Mafunzo hayo, Giffrin Mwakapuje, alisema mafunzo hayo yanaendeshwa na serikali chini ya ufadhiri wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto (UNICEF), ambalo pia linatekeleza miradi mingine kwenye mikoa hiyo.

Alisema mafunzo hayo yanatarajiwa kufanyika katika mikoa mbalimbali nchini kwa maofisa wa majeshi hayo pamoja na wadau wengine wanaohusika kwenye utoaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi.

"Sio kwamba tumeanza kwenye mikoa hii kwa sababu pengine ndiyo inaongoza kwa kuwa na makosa mengi ya ukatili dhidi ya watoto hapana, bali tumeichukua mikoa hii kama sehemu ya kuanzia na tutaendelea kuyatoa nchi nzima," alisema Mwakapuje.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema yatawasaidia kuwa mahiri katika kushughulikia matatizo ya watoto ikiwamo ukatili na unyanyasaji wa kundi hilo pamoja na makundi mengine ya watu wasiojiweza.

Mmoja wa maofisa hao, Jesca Chinuka, ambaye ni askari kutoka katika Mkoa wa Iringa, alisema mafunzo hayo yatamsaidia kutoa elimu kwa jamii kuhusu kuzuia matukio ya watoto kukinzana na sheria.

Alisema tatizo kubwa linalokabili jamii ni wazazi kutoelewa maana ya mtoto kukinzana na sheria na hivyo huwa wanalazimika kuwapeleka kwenye vituo vya polisi na magerezani.



Maofisa wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mbeya, wakifanya usafi kwa kuondoa mafuta yaliyomwagika barabarani kwenye mteremko wa mlima Mbalizi wiki iliyopita, baada ya lori la mizigo kufeli breki na kuyagonga magari madogo matatu na bajaji na kusababisha kifo na majeruhi. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Wanahabari washauriwa kumuenzi Mkapa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANDISHI wa habari nchini wameshauriwa kumuenzi kwa vitendo aliyekuwa rais wa awamu ya tatu, Hayati Benjamini Mkapa, kwa kuzingatia maadili ya taaluma hiyo ikiwamo kuandika vitu vyenye ukweli.

Ushauri huo ulitolewa jijini Mbeya juzi na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harison Mwakyembe, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari wa mkoa wa Mbeya kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu wizara yake.

Alisema Hayati Mkapa ni miongoni mwa waliowahi kuwa wandishi nguli wa habari, ambao walikuwa wanaandika vitu vyenye ukweli na ambavyo vilikuwa vinalisaidia taifa hasa alipokuwa mhariri wa vyombo vya habari vya Serikali.

"Huyu ndiye aliyeipa heshima taaluma yetu pale alipoonyesha kuwa wandishi wa habari wana uwezo mzuri wa kuongoza taifa, alifanya vizuri sana kwenye taaluma hii, wakati tunaomboleza kifo chake tunatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya taaluma yenyewe," alisema Dk. Mwakyembe.

Alisema Hayati Mkapa ndiye aliyekihamisha kilichokuwa Chuo cha Uandishi wa -Habari Tanzania (TSJ) kutoka wizarani kwenda kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (sasa ni Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma (SJMC).

Alisema baada ya kukihamisha alimteua yeye (Mwakyembe) kuwa mwenyekiti wa kwanza wa bodi, na kwamba kuanzia hapo ndipo taaluma ya habari ilianza kukua nchini.

Katika hatua nyingine, Waziri Mwakyembe aliwataka wandishi wa habari ambao hawana elimu kuanzia Diploma kuendelea kujiandaa kupata sifa hiyo kabla utekelezaji wa Sheria ya Huduma ya Habari ya Mwaka 2016 haujaanza. Alisema kuanzia mwakani hakuna mwandishi mwenye elimu chini ya diploma ambaye atatakiwa kufanya kazi ya habari, hivyo aliwataka hata wamiliki wa vyombo vya habari kuendelea kuwasomesha wafanyakazi wao mpaka wapate sifa hiyo.

Baadhi ya wandishi wa habari waliiomba Serikali kuwasaidia wanahabari wasio na elimu ya Diploma kupata sifa hiyo kwa maelezo kuwa baadhi yao wanashindwa kusoma kwa sababu hawana uwezo wa kiuchumi.

Mwenyekiti wa Klabu ya Wandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya (MBPC), Festo Sikagonamo, aliiomba Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kulegeza msimamo wa kuwaondoa wandishi wasiokuwa na diploma na badala yake iwasaidie kupata sifa hizo.

Alisema MBPC imeandaa mpango mkakati wa miaka mitano ambao moja kati ya malengo yake ni kuwaendeleza wanachama wake na masomo ili wapate sifa ya diploma ambayo ndiyo inayotambuliwa kwa mujibu wa sheria ya huduma ya habari. "Kinachotukwamisha ni uwezo wetu kuwa mdogo kiuchumi, hivyo tunaiomba Wizara yako, itusaidie hata kupata wataalamu watakaotushauri namna ya kupata fedha za kutekeleza jambo hili," alisema Sikagonamo.

Naye Emmanuel Lengwa, aliiomba Wizara kusogeza baadhi ya huduma zake mikoani ikiwamo upatikanaji wa vitambulisho vya wandishi (Press Card) badala ya kupatikana Dodoma na Dar es Salaam, kwa maelezo kuwa hatua hiyo itawapunguzia wandishi gharama.



# 'Uongozi wa Mkapa ulikuwa na msimamo usioyumba'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAWAZIRI wastaafu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Zanzibar ambao walifanya kazi na Rais mstaafu marehemu Benjamin Mkapa, wamemlilia kiongozi huyo na kusema kuwa katika uongozi wake alikuwa na msimamo usioyumba.

Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani na baadaye Waziri wa Nchi anayeshugulikia Habari, Ali Ameir, amemuelezea marehemu Benjamin Mkapa kuwa alikuwa ni mtu wake wa karibu na alikuwa muumini wa Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano na hakuwa tayari kuona kiongozi anayechezea tunu hizo. "Alipoingia madarakani mpaka mwaka 1995 aliniteua Waziri wa Mambo ya Ndani...ni rafiki yangu sote tulikuwa waandishi wa habari alikuwa Mhariri wa Uhuru na Nationalist," alisema Ameri wakati akizungumza na Nipashe.

Aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango akiwa pia Mbunge wa Jimbo la Makunduchi, Abdisalami Issa Khatib, alimtaja marehemu Mkapa kuwa rais aliyemchagua na kushika wadhifa huo kuwa ni mbunifu katika masuala ya uchumi na fedha ingawa sio taaluma yake.

Alisema kazi yake ya kwanza wakati alipoingia madarakani ni kukuza uchumi na kufanya mazungumzo tena na taasisi za fedha za kimataifa ambazo zilisitisha misaada yao kwa madai nchi haikuwa makini katika ukusanyaji wa kodi.

"Tulipoingia madarakani mwaka 1995 baadhi ya taasisi za fedha zilitususia misaada kwa sababu ya kushindwa kusimamia masuala ya kodi...Mkapa alianzisha Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA) na mazungumzo na taasisi za fedha yalianza na hapo walianza kutukubali," alisema. Aliyekuwa Mbunge wa jimbo la Wawi kwa tiketi ya CUF Hamad Rashid Mohamed, amemtaja marehemu Mkapa kuwa ni kiongozi aliyefanya kazi pamoja katika Serikali ya Mwalimu Julius Nyerere, yeye akiwa Naibu waziri wa Mambo ya Ndani hadi serikali ya rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi, akiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi. Alisema baada ya kutokea mauaji ya Pemba katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2000, Mkapa alisaidia kuwapo kwa maridhiano ya kisiasa yaliyofanya kuwapo kwa muafaka wa kisiasa.

Mohamed alisema hatomsahau Mkapa ambaye baadaye baada ya kuomba ridhaa kutoka katika chama cha CUF alimteua kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kupitia nafasi 10 za uteuzi wa rais.

"Mimi katika kipindi cha Rais mstaafu Mkapa nilikuwa mtu pekee kutoka upinzani niliyeteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano baada ya kufanya kazi kubwa ya kuleta maridhiano ya kisiasa kufuatia kuchafuka kwa hali ya kisiasa Pemba baada ya uchaguzi mkuu wa 2000," alisema.



Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi 'A' Unguja, Amour Mussa, akipokea kitambulisho chake kipya kutoka kwa mfanyakazi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Washangaa wanawake wenzao kutowaunga mkono

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANAWAKE wa vyama tofauti vya kisiasa Zanzibar waliogombea nafasi ya Ubunge, Uwakilishi na Udiwani wamesema wanashangazwa kuona wanawake wenzao hawajawa tayari kuwaunga mkono kuwa viongozi.

Wakizungumza na Nipashe baada ya kuangushwa katika kura za maoni walisema, wajumbe wengi wanaopiga kura za maoni ni wanawake, lakini wameshindwa kuwatetea wanawake wenzao.

"Kwa kweli hawa wajumbe ni watu wabaya sana, licha ya elimu inayotolewa kuhusu ushiriki wa wanawake katika ngazi za uamuzi, lakini wameshindwa kututetea wanawake wezao," alisema Halima Juma (siyo jina halisi) aliyegombea nafasi ya udiwani.

Alisema wanawake wengi wameanguka katika kura za maoni na hatimaye nafasi hizo zimeshikiliwa zaidi na wanaume.

Bahati Issa aliyegombea nafasi ya udiwani, alisema bado elimu ya uhamasishaji kuhusu ushiriki wa wanawake katika uongozi inahitajika hasa kwa wajumbe wanaopiga kura za maoni.

Alisema wengi wa wajumbe hao wamenunuliwa na wagombea wanaume hali ambayo imesababisha kutowaunga mkono wanawake waliogombea. Asha Bakari kutoka Chama cha ACT-Wazalendo, alisema kuwa wanawake wanakabiliwa na changamoto nyingi katika kupata nafasi za uongozi majimboni.

Alisema rushwa ni moja ya kikwazo kinachowakwamisha kupata nafasi katika kura za maoni.

Kadhalika, alifafanua kuwa wanawake wanapata vitisho kutoka kwa wanaume wanapothubutu kugombea nafasi ya uongozi majimboni.

Raisa Abdallah, alisema imefika wakati sasa wanawake wabadilike kwa sababu rafiki wa mwanamke ni mwanamke hivyo ni vyema wakaungana. "Wapiga kura wengi wao ni wanawake, lakini sisi wenyewe tumekua tukiangushana... naomba wanawake tubadilike anaposimama mwanamke kuomba nafasi kumuunga mkono na kumpigia kura," alisema Raisa ambaye aligombea uwakilishi kupitia chama hicho.

# ZEC yaombwa kuondoa gharama kitambulisho kinapopotea

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BAADHI ya wanawachi waliofika kuchukua vitambulisho vyao vya kupigia kura katika vituo maalum vilivyowekwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), wameiomba Tume hiyo kuondoa gharama ya kulipia kitambulisho hicho kwa wale ambao wamepoteza cha zamani.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, walisema kuwa baadhi ya wananchi wamepoteza vitambulisho vyao vya awali vya kupigia kura na wanapofika kituoni kuchukua kipya hutakiwa walipie Sh. 5000.

Alisema kupiga kura ni haki yao ya kidemokrasia hivyo ni vyema gharama hiyo ikaondolewa ili kila mwenye sifa aweze kuitumia haki yake.

"Wananchi wengi waliopoteza vitambulisho vyao vya zamani wameshindwa kulipia shilingi elfu tano kwa sababu sio kila mwananchi anaweza kumudu gharama hiyo," alisema Abedi Suleiman.

Abedi aliiomba ZEC kuondosha gharama hiyo na kutafuta njia nyengine mbadala ambayo itakua ni nafuu kwa wananchi waliopoteza vitambulisho vyao vya zamani vya kupigia kura ili kuweza kupatiwa vitambulisho vipya.

Naye Ofisa Habari wa ZEC, Jaala Makame, alisema kuwa gharama ya Sh. 5,000 kwa waliopoteza kitambulisho cha zamani cha kupigia kura utaratibu uliowekwa na kwa mujibu wa kanuni ya Tume ya Uchaguzi.

"Gharama hiyo ni jambo la kawaida hata unapopoteza Kitambulisho cha Taifa unatakiwa ulipie Sh. elfu ishirini ili uweze kupata kitambulisho kipya," alisema.

Utoaji wa vitambulisho vipya vya kupigia kura umemalizika jana, kwa ambao hawakwenda kuchukua vitambulisho vyao watatakiwa kwenda katika Ofisi za Tume za wilaya kwa ajili ya kuchukua.

# Kigwangalla, Ngasongwa wamzungumzia Mkapa

**Elizabeth Zaya na Salome Kitomari**

BAADHI ya viongozi wa sasa na wa zamani serikalini, wamemuelezea Hayati Benjamini Mkapa, kuwa amefanya mambo ambayo yanapaswa kuigwa na Watanzania.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Khamisi Kigwangalla, alisema mwezi mmoja uliopita alizungumza na Mkapa kwa zaidi ya saa moja, baada ya kiongozi huyo kumpigia kuhusiana na kauli za alivyojipanga kuhakikisha sekta ya utalii haiyumbi baada ya kuathiriwa na ugonjwa wa corona.

"Mimi sikuwahi kupata bahati ya kuzungumza naye kwa muda mrefu kama siku hiyo. Kwa hiyo ilikuwa bahati nilipata busara zake kwa mara ya mwisho na nilijifunza,nilichota hekima na busara kutoka kwake siku hiyo na namna ambavyo pamoja na kwamba ni mstaafu, lakini bado alikuwa anatumia uwezo wake na kufikiria namna ya kulisaidia taifa lake,"alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Kigwangalla, yapo mambo mengi ya kujifunza kutoka kwa Mkapa ikiwamo uzalendo kwa nchi yake na uwazi, kutokuwa na papara na uamuzi, ubunifu, kuweka mifumo inayodumu milele.

"Ametufundisha kwamba ukiwa kiongozi lazima ujue kwamba kuna kukosea pia na ukatambua kwamba umekosea na ukakiri na siyo kwa sababu ya nafasi yako ukajiona kwamba uko sahihi na tunajua kila jambo."

Naye, Waziri wa zamani wa Viwanda na pia Maliasili na Utalii, Juma Ngasongwa, aliyehudumu katika serikali ya Mkapa, alisema katika uongozi wake alipenda kutenda haki na alikuwa muwazi endapo unakosea au unafanya vizuri.

"Niliwahi kufanya japo ambalo hakulipenda aliniambia ukweli, lakini pia nilipofanya vizuri alinipongeza na alikuwa hapendi pia mtu kuonewa na hili lilinifanya nimheshimu mpaka sasa,"alisema Ngasongwa.

Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya katika kipindi cha Mkapa, Baraka Konisaga katika wilaya za Temeke na Ukerewe, alisema Mkapa alipenda kusisitiza kufanya kazi kwa juhudi, weledi na uaminifu.

Aidha, alisema alitumia anatumia mbinu mbalimbali kufuatilia utendaji wa wasaidizi wake bila hata wao kujua.

"Mimi ni miongoni mwa watu ambao wakati Mkapa anaanzisha mpango wa ujenzi wa shule za Kata, nilishiriki kusimamia, alikuwa anatufuatilia utendaji wetu kila mmoja hata bila kujua, alikuwa ni mchapakazi na alipenda haki sana," alisema Konisaga.



Kaimu Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo TARI Naliendele, Dk. Fortunus Kapinga, akionesha bibo alilochuma katika shamba la mfano la korosho lililopo Viwanja vya Maonesho Nanenane Ngongo mkoani Lindi mwishoni mwa wiki, alipokuwa akikagua mashamba hayo yakiwa ni maandalizi ya maonesho hayo Kanda ya Kusini yatakayoanza Agosti 1, 2020. **PICHA: NA DOTTO MWAIBALE**

# THRDC yataka urekebishaji sheria kandamizi

**Na Beatrice Shayo**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umewataka wadau kushirikiana katika kuhakikisha haki za msingi na sheria kandamizi zinafanyiwa marekebisho ili kuwapo uhuru wa kujieleza.

Hayo yamesemwa na Mratibu wa Kitaifa wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, mwishoni mwa wiki wakati akifunga mafunzo ya siku tatu yaliyokutanisha waandishi wa habari, wanasheria na wadau mbalimbali wa haki za binadamu.

"Uhuru wa kujieleza ndio msingi wa haki zingine zote nchini, hivyo ni muhimu wadau hao kushirikiana kutokomeza sheria zote kandamizi zinazozuia kuwapo kwa uhuru huo," alisema Olengurumwa.

Olengurumwa alisema uhuru wa kujieleza isiwe tu kwa wanasheria ama waandishi wa habari, uwe ni kwa wananchi wote.

"Ninyi waandishi wa habari na wanaharakati mmekuwa mkitafuta habari ili kuzitoa, hivyo mara nyingi uhuru wa kujieleza unaonekana kama ni wa kwenu peke yenu kuupata, lakini kimsingi, uhuru wa kujieleza ni haki ya kila mtu.

"Mfano mtoto akifanyiwa ukatili ana haki ya kueleza kilichotokea na huo ndio uhuru wa kujieleza, mtu akifanyiwa kitua ambacho si kizuri na kutaka kuongea huo ndio uhuru tunaosema," alisema.

Aidha, alisema ili mtu aweze kutetea haki za watu wengine, ni muhimu kuwapo kwa uhuru wa kujieleza na kuongeza kuwa sehemu yoyote ambayo haina jambo hilo ni rahisi haki za jamii kuminywa.

Alisema anaamini kuwa wale waliofanikiwa kushiriki katika mafunzo haya watakwenda kuibadilisha jamii, huku wanasheria kuwa na uwezo kwa kusimamia na kutetea na hatimaye kushinda kesi zote za waandishi na uhuru wa vyombo vya habari. Mjumbe wa bodi ya THRDC, Keneth Simbaya, alisema mafunzo yaliyotolewa ni muhimu kwa wanasheria hasa katika kuwajengea uwezo wa kusimamia kesi za kutetea haki za binadamu.

Simbaya aliwataka washiriki kuhakikisha mafunzo wanayatumia kwenda kusaidia jamii kwenye utetezi wa kesi mbalimbali zinazowakabili.

## Waomba REA kuwaunganishia umeme

**Na Welingtone Masele,** KALIUA

BAADHI ya wananchi wa Kijiji cha Kagera, Kata ya Kashishi, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua wameomba Wakala wa Umeme Vijijini (REA), wilayani humo kuwawashia umeme, wote waliokwisha funga mtandao wa umeme kwenye nyumba zao ili waanze kunufaika na huduma hiyo.

Wananchi hao wamesema zaidi ya nusu ya wakazi wa kijiji hicho wameshaunganishiwa nyaya za umeme katika nyumba zao, wanachosubiri ni kuwashiwa ili waanze kuutumia.

Mwananchi Kulwa Buganga Ndomelo (49), alisema nishati ya umeme ni muhimu katika shughuli zao za kila siku wanachosubiri kwa sasa ni huduma hiyo kwa hamu kubwa.

Alisema wataalamu wa REA wameshafikisha nguzo katika kijiji hicho na waya zimeshafungwa, lakini wanashangaa kutounganishiwa kwenye nyumba zao.

"Tunahitaji sana umeme hapa kijijini, tunaomba REA watusaidie ili kufanikisha shughuli zetu za uzalishaji mali na usalama wakati wa usiku, tayari tulishamaliza kufanya 'wiring' (kuweka waya) katika nyumba zetu tunawasubiri wao tu," alisema.

Didas Kasaba, mkulima mkazi wa kijiji hicho alisema umeme huo utaharakisha maendeleo ya kijiji hicho kwa kuwa shughuli zao nyingi zinahitaji nishati hiyo mfano mashine za kusaga na kukoboa, saluni za kunyoa nywele na kazi za uchomeleaji.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Lameck Mtundu, alikiri kuwa nguzo za REA zimeshafika kijijini hapo na wananchi wengi wameshafanya wiring, kinachosubiriwa ni kuingiziwa umeme katika nyumba zao.

## Bei ya ufuta yapanda kiduchu

**Na Said Hamdani,** LINDI

BEI ya zao ufuta inaendelea kuimarika mkoani Lindi kufuatia wanunuzi wanaojitokeza kuongeza bei kutoa Sh. 1,820 kwenye mnada uliopita hadi kufikia Sh. 1,892.

Mnada huo ulifanyika jana Kijiji cha Naikiu, Kata ya Nanjirinji, Wilaya ya Kilwa, chini ya usimamizi wa Mwenyekiti wa chama kikuu cha Lindi Mwambao, Rashidi Masudi.

Akitangaza bei Ofisa Ushirika, Richard Lengo, alisema kampuni kumi zilizijitokeza kununua ufuta huo uliopo kwenye maghala ya Nangurukuru, Bucco na Ilulu Mtama yaliyopo Kilwa.

Lengo alisema kiwango cha juu kilichofikiwa na wafanyabiashara hao ni Sh. 1,892 kwa kilo moja na cha chini ni Sh. 1,857.

Alisema ghala la Nangurukuru lina tani 908 na kilo 325, Bucco (241 na kilo 264) wakati Ilulu Mtama lina tani 23 na kilo 224. Kampuni ya RBST imenunua tani 600 na tani 573 zilizobaki zikinunuliwa na kampuni tisa zilizobaki.

Hadi kufikia jana Mkoa wa Lindi ulifanya minada 14 kwa vyama vikuu viwili vya Lindi Mwambao na Runali.

## HABARI KIMATAIFA

# China yaripoti maambukizi mapya 46 ugonjwa corona

**BEIJING,** China

TUME ya Afya nchini China imesema maambukizi mapya ya virusi vya corona yameongezeka kutoka 34 hadi 46 kwa siku.

Imesema miongoni mwa maambukizi hayo mapya, 22 yalikuwa katika jimbo la magharibi ya mbali la Xinjiang.

China iliripoti kesi mbili mpya za watu walioonesha dalili, ikiwa ni chini kutoka watu 74 siku moja kabla.

Tume hiyo pia imesema hadi siku ya Jumamosi, China ilikuwa na kesi za maambukizi ya virusi vya corona 83,830 zilizothibitishwa kwamba vifo kutokana na ugonjwa huo vimefikia watu 4,174,437.

**Katika siku 12 zilizopita, idadi ya maambukizi mapya yanaripotiwa kila siku imepita 60,000.**

Marekani siku ya Jumamosi ilirekodi maambukizi mapya ya watu 68,212 katika saa 24 yaliyopita, Chuo Kikuu cha John Hopkins kiliripoti katika hesabu zake za kila siku.

Hii inafikisha jumla ya idadi ya kesi za maambukizi katika Taifa hilo lililoathirika zaidi duniani kufikia 4,174,437.

Baada ya kupungua katika viwango vya maambukizi mwishoni mwa robo ya kwanza ya mwaka huu, Marekani imeshuhudia ongezeko la maambukizi ya virusi vya corona, hususani katika majimbo ya kusini na magharibi mwa nchi hiyo kama Califonia, Texas, Alabama na florida.

Katika siku 12 zilizopita, idadi ya maambukizi mapya yanaripotiwa kila siku imepita 60,000.

Wanasayansi wanakubaliana kuwa ongezeko katika viwango vya vifo linafuatia ongezeko la maambukizi kwa wiki tatu hadi nne. Jumla ya vifo kila siku kwa nne zilizopita imefikia 1,000. **DW**



Kiongozi wa Korea kaskazini, Kim Jong Un (wa tatu kutoka kushoto), akiongoza kikao maalum cha kamati ya uongozi kuzungumzia maambukizi ya virusi vya corona. **PICHA: REUTERS**

# Kenya kuanza majaribio dawa corona

**NAIROBI,** Kenya

WAGONJWA 10 nchini Kenya wameanza kushiriki katika jaribio la kupata dawa ya corona katika hospitali ya Chuo Kikuu cha Aga Khan.

Wanaoshiriki katika jaribio hilo ni wagonjwa ambao wamepatikana na ugonjwa wa corona na CT scan yao inaonyesha kuwa wameathirika na nimonia inayohusiana na corona na wanahitaji oksijeni.

Hata hivyo, Madaktari watatathmini ufanisi na usalama wa Actemra (tocilizumab) dawa iliyotengenezwa na kampuni ya Roche katika jaribio hilo. Daktari Reena Shah, mtaalamu wa magonjwa yanayoambukizwa kwa haraka ameitaja kama wakati muhimu nchini Kenya.

"Huu ni wakati wa furaha nchini Kenya na katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Aga Khan kwamba tunaweza kushiriki katika jaribio la kliniki la kimataifa ambalo linajaribu ufanisi wa dawa hii kwa wagonjwa wetu hapa," alisema Dk. Reena Shah na kuongeza.

"Hapa ndipo tunachangia maarifa na uzoefu juu ya uwezo wetu na matokeo ya wagonjwa wetu kwa jamii ya kimataifa," alisema.

Alisema dawa ya Tocilizumab, ambayo inatumika katika matibabu ya saratani na kwa ugonjwa wanaougua arthritis, inatumika sasa katika jaribio la ugonjwa wa corona kwamba itamzuia mtu kuwa na ugumu wa kupumua.

Katika jaribio hili, hakuna atakayejua ni mgonjwa yupi aliye kwenye dawa ya Tocilizumab na ni nani yuko kwenye dawa ya kutuliza (placebo). Matokeo ya awali ya utafiti huo yatajulikana baada ya miezi mitatu.

Mbali na Kenya jaribio hilo linafanyika katika mataifa ya Afrika Kusini, Brazil, Mexico na Peru.

Watafiti wa Chuo Kikuu cha Michigan waligundua kuwa uchunguzi uliofanywa kwa wagonjwa 154 wenye ugonjwa wa corona waliohitaji kupewa oksijeni, dawa hiyo iliripotiwa kupunguza vifo kwa asilimia 45.

Ni miezi mitatu tangu Shirika la Afya Duniani (WHO) kutangaza kwamba kusambaa kwa virusi vya corona kumesababisha janga.

Tangu Machi 11, mwaka huu tafiti mbalimbali zimezinduliwa kuhusu tiba ya ugonjwa huo.Ukweli ni kwamba tayari hatua kubwa zimeafikiwa katika utafutaji wa tiba ya maradhi hayo.

Maabara zilizopo katika mataifa tofauti duniani zimeanza kuchunguza takriban tiba 150. Baadhi yake tayari zilikua zikiuzwa katika maduka ya dawa na sasa zinafanyiwa vipimo iwapo zinaweza kutibu ugonjwa huo.

Hata hivyo, WHO imekuwa ikizifanyia majaribio dawa zinazoleta matumaini kwa mgonjwa. **BBC**

## Corona yaua watu 572 Afrika Kusini kwa siku

**JOHANESBURG,** Afrika Kusini

WATU 572 wamepoteza maisha kutokana na kuugua virus vya corona kwa kipindi cha saa 24 zilizopita Afrika Kusini.

Kadhalika, kuna wasiwasi kuwa huenda idadi ya waliopoteza maisha nchini humo kutokana na virusi vya corona ni kubwa zaidi kuliko takwimu zinavyoonesha. Lakini watafiti kutoka baraza la utafiti wa tiba nchini Afrika Kusini wamesema kuwa idadi ya waliopoteza maisha ni kubwa zaidi kuliko kawaida, wakisema kuwa maelfu ya vifo vitokanavyo na ugonjwa wa corona huenda havikuripotiwa.

Mpaka sasa, takwimu rasmi zinaonyesha kuwa karibu watu 6,000 walipoteza maisha kutokana na ugonjwa wa corona. Lakini tafiti za miezi miwili iliyopita zilionesha kuwa kumekuwa na vifo 17,000 zaidi kuliko kawaida. Watafiti walisema kuna vifo 11,000 ambavyo havijaelezwa.

Watafiti hao wanakisia kuwa vingi kati ya hivyo inawezekana kuwa vinahusiana na ugonjwa wa corona kama wale waliopoteza maisha wakiwa nyumbani na vifo vingine ambavyo havijaripotiwa.

Lakini kumekuwa na maoni kuwa raia wa Afrika Kusini wanaepuka kwenda hospitali kwasababu hakuna nafasi, au wasiwasi wa kupata maambukizi. **BBC**

## Wanasheria waishtaki serikali ya Rais Trump

**WASHINGTON,** Marekani

MAKUNDI mbalimbali ya wanasheria yamefungua mashtaka dhidi ya serikali ya Marekani kujaribu kuzuia kuondolewa nchini watoto waliokuwa wamefungiwa katika vyumba vya hoteli.

Serikali ya Marekani ilitoa tamko la dharura ikisema imeamua kufanya hivyo kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Wamiliki wa Hoteli ya Hampton Inn & Suites huko McAllen, Texas, walisema kuwa wamesitisha kupokea maombi ya wateja wapya kuingia katika vyumba hivyo ambavyo watoto walikuwa wamefungiwa ndani.

Vyombo vya Uhamiaji na Forodha vimethibitisha kuwa watoto wote wameshaondolewa hotelini, siku mbili baada ya shirika la Habari la Associated Press kuripoti kuwa hoteli hiyo ni kati ya hoteli tatu zilizotumika zaidi ya mara 200 kuwashikilia watoto ambao wengine ni chini ya umri wa mwaka mmoja.

Wakili wa Jumuiya ya American Civil Liberties, Lee Gelernt, iliyofungua kesi kwa niaba ya Mradi wa Haki za Kiraia Texas alisema kufungua mashtaka kwa niaba ya watoto wasiotajwa majina yao ni muhimu.

Takwimu za serikali zilizokusanywa na Shirika la Habari la AP zinaonyesha watoto walishikiliwa mara 123 katika Hoteli ya McAllen, Aprili na Juni. **VOA**

HABARI MICHEZO

# PSG YATHIBITISHA MBAPPE KUUMIA



**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain imethibitisha Kylian Mbappe ameumia katika kifundo cha mguu wa kulia.

Fowadi huyo aliumia wakati akikabana na Loic Perrin, ambaye alitolea nje kwenye ushindi wa PSG wa 1-0 dhidi ya Saint-Etienne katika fainali ya Coupe de France, Ijumaa.

Nyota huyo wa timu ya taifa ya Ufaransa alionekana kuwa na magongo wakati akishangilia ushindi na wachezaji wenzake na alifanyiwa uchunguzi wa kina Jumamosi.

PSG ilitangaza katika taarifa yake kwamba "ameumia katika kifundo chake mguu wa kulia."

Mbappe anaweza kuwa nje ya dimba kwenye mchezo wa robo fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya wakati PSG itakapoivaa Atalanta, ambapo itafanyika mjini Lisbon, Agosti 12.

Pia anatarajia kuukosa mchezo wa fainali ya kombe la Coupe de la Ligue dhidi ya Lyon, Julai 31.

Mapema Jumamosi, Mbappe aliposti kwenye Twitter: "Nimeamka kama mshindi. Shukrani kwa ujumbe wenu, kwa hakika imenigusa."

PSG pia ilithibitisha kwamba, Thilo Kehrer atakuwa nje ya dimba kwa siku nne au tano baada ya kuumia kiuno.

Hata hivyo, Abdou Diallo na Juan Bernat wanajiandaa kurudi kwenye mazoezi leo Jumatatu.

# Ibrahimovic akataa kustaafu soka

**MILAN,** Italia

STRAIKA wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic anaonekana kuondoa uwezekano wa kustaafu, akisisitiza: "Bado najifua!"

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona, Paris Saint-Germain na Manchester United alijiunga na Milan kwa mkataba wa muda mfupi Desemba, lakini kuna shaka juu ya majaliwa yake ya kuendelea kukaa hapo.

Kocha mkuu wa Rossoneri hao, Stefano Pioli anataka kumbakiza mchezaji huyo kwenye dimba la San Siro.


Imebainisha kwamba Ibrahimovic anaweza kustaafu wakati msimu huu 2019-20 wa Serie A utakapomalizika Agosti, ikiwa ni miezi miwili kuelekea kuazimisha siku yake ya kuzaliwa akitimiza miaka 39.

Hata hivyo, kupitia video iliyowekwa kwenye Instagram Jumamosi, Ibrahimovic alisema: "Hivyo, mnafikiri kwamba nimemaliza, kwamba kipindi changu cha kucheza soka kitafikia mwisho. Haunijui.

"Katika maisha yangu lazima nipambane. Hakuna mtu anayeniamini mimi, hivyo natakiwa kujiamini mimi mwenyewe.

"Kuna baadhi watu walitaka kuniondoa, lakini ndio wananifanye niwe imara. Wengine walitaka kunipoteza mimi; na hilo ndilo limenifanya mimi kuwa imara zaidi.



# Lingard: Greenwood atafanya makubwa sana kwa Man Utd

**MANCHESTER,** England

JESSE Lingard anajiamini mchezaji mwenzake wa Manchester United, Mason Greenwood atabakia kuwa mnyenyekevu na kuendelea kujijenga zaidi kwenye kasi ya ufungaji kama alivyofanya msimu huu.

Greenwood amefurahia msimu huu wa 2019-20, na kuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer licha ya kuwa na umri wa miaka 18 pekee.

Fowadi huyo amefunga mabao 17 katika mashindano yote, akifikia rekodi ya Wayne Rooney, George Best na Brian Kidd ya kufunga mabao mengi akiwa na umri mdogo, na amekuwa akianza mara kwa mara tangu tangu ligi hiyo iliporudi Juni.

Mafanikio yake ya haraka yameibua matarajio mengi kwake, kwa klabu na nchi yake, lakini Lingard anaamini mhitimu mwenzake huyo wa akademi ya soka ana mtazamo chanya wa kuendelea kuimarika.

"Tangu alipoanza mazoezi na timu ya kwanza, amefanya mambo ya kuvutia," amesema Lingard - ambaye ameanza katika mechi tisa tu msimu huu akiiambia Sky Sports.

"Ingawa ni kijana, lakini ameonekana kuimarika na ana nafasi ya kutamba zaidi kwa siku za usoni kwa kufunga mabao na kutoa pasi za mwisho.

"Ameongeza mchango mkubwa sana kwa timu na kwa uhakika kabisa atasaidia sana timu na kuwa mchezaji muhimu zaidi kwa kikosi chetu."

# Guardiola ajipanga kuitoa Real Madrid

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola haamini kama Manchester City inahitaji kufikiria namna ilivyotolewa kwenye Ligi ya mabingwa msimu uliopita na ilivyoshindwa kutetea taji la Ligi Kuu, wakati wakijiandaa kuivaa Real Madrid.

City ina malengo ya kulitwaa taji la Ulaya kwa mara ya kwanza msimu huu, lakini lazima iwaondoe kwanza mabingwa mara 13 wa Ligi ya mabingwa Ulaya, Madrid, ambapo waliwafunga 2-1 kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya 16.

"Ninachotaka ni kucheza mchezo mzuri," alisema Guardiola. "Kwa uhakika kabisa hii ni fainali. Kwa upande wetu, kwa Madrid, ni fainali.

"Mpango wetu ni kuhakikisha hatufanyi makosa na kujaribu kucheza soka la kuvutia kadili itakavyowezekana.

"Nafikiri kile kilichotokea mwanzo kitatufanya sisi tucheza kwa ubora zaidi. Kile kilichotokea awali kimeshapita. Wakati mwingie unatakiwa kukubali kile kilichotokea.

"Ni maisha. Hatukuwa sawa, kwa sasa akili yetu ni kuhakikisha tunacheza kwa bidii na nguvu kuhakikisha kwamba tunasahau yaliyopita.

"Hamasa yetu ni kusonga mbele, kujithibitishia sisi wenyewe tunaweza kucheza mchezo mzuri na kuwafunga Real Madrid. Hiki ndio kitu pekee tunachoweza kufanya.

"Kile kilichotokea mwanzo hakitatupa nafasi kwa mechi yetu ijayo, kwani mchezo wetu dhidi ya Real Madrid ni wa muhimu zaidi na tutatakikwa kuingia kwa tahadhari kubwa."






# NAPOLI HAIJAPATA OFA YOYOTE KWA KOULIBALY

**NAPLES,** Italia

NAPOLI haijapokea ofa yoyote ya maana mezani kwao kwa ajili ya Kalidou Koulibaly, Mkurugenzi wa soka, Cristiano Giuntoli amebainisha.

Mlinzi huyo wa kati wa kimataifa wa Senegal, alikuwa akihushwa na uhamisho wa kwenda Manchester City, ambao wamemaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu ya England nyuma ya Liverpool.

City ilifanikiwa katika rufaa yake ya kufungiwa katika mashindano ya Ulaya na inaweza kuwa klabu itakayomvutia Koulibaly.

Hata hivyo, Napoli haina haraka ya kumuuza, ingawa dili lolote linaweza kuisaidia timu kupata fedha na kujijenga kwenye safu yake ya ushambuliaji kwa msimu ujao.

Giuntoli aliiambia DAZN: "Kwa wakati huu hakuna ofa yoyote mezani kwetu. Hatuna haraka kuamua kwa sasa."

Koulibaly mwenye umri wa miaka 29, anaweza kuondoka, huku Napoli ikiangalia uwezekano wa kuimarisha safu yake ya ushambuliaji kwa kutaka kumsajili Victor Osimhen kutoka Lille, huku straika huyo wa Nigeria akithibitisha kuwaniwa.

# *Capello: Jezi ya Madrid imemuathiri Hazard*

**MADRID,** Hispania

FABIO Capello anaamini mzigo wa kuvaa jezi ya Real Madrid umechangia Eden Hazard kushindwa kutamba kwenye msimu wake wa kwanza pale Santiago Bernabeu msimu huu.


Winga huyo wa zamani wa Chelsea, Hazard alinunuliwa kwa euro milioni 100 kwenda kwa miamba hao wa Hispania mwanzoni mwa msimu huu, lakini majeruhi ya mara kwa mara yameifanya kutokuwa na wakati wa kuvutia kwa Los Blancos.

Ameanza katika mechi 14 na amecheza jumla ya mechi 16 kwenye LaLiga, akifunga bao moja na kutoa pasi za mwisho tatu.

Kiwango hicho ni cha chini zaidi ikilinganishwa na wakati wake akiwa Chelsea katika msimu wake wa mwisho, ambapo alifunga mabao 16 na kutoa pasi za mwisho 15 katika mechi 37 za Ligi Kuu ya England, ikiwemo kuanza mara 32.

"Bila shaka hajawa sawa kama alivyokuwa Chelsea," amesema kocha huyo wa zamani wa Madrid, Capello akiliambia gazeti la Marca. "Amekuwa kwenye majeruhi kwa muda mrefu, na bado hajazoea ligi.

"Mara zote nimekuwa nikimfikiria yeye kama mchezaji mkubwa. Lakini lazima tuwe wakweli, jezi ya Real Madrid ni zito sana kwa Hazard na amezama mwaka huu. Ni wazi kwamba msimu ujao utakuwa bora kwake."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CONTE AFURAHISHWA MESSI KUHUSISHWA INTER

●●● Asema hadhani kama kuna mtu kichaa duniani ambaye hatamhitaji, lakini kwa hali jinsi ilivyo...

**MILAN,** Italia

KOCHA Mkuu wa Inter Milan, Antonio Conte, ameelezea mazungumzo ya uwezekano wa ujio wa nahodha wa Barcelona, Lionel Messi kama "ndoto ya soka", ingawa amekaribisha uhamisho huo.

**Majaliwa ya Messi yametawala vyombo vya habari kuelekea mwishoni mwa msimu huu 2019-20 na mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or yupo tayari kuondoka pale Barca mkataba wake utakapomalizika mwakani.**

Awali alihusishwa na Inter, na ripoti za hivi karibuni kwamba baba yake mzazi Messi amenunua nyumba jijini Milan wiki hii, imekoleza moto uvumi wa yeye kuhamia kule San Siro.

Conte alipoulizwa kuhusu Messi baada ya Inter kuibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Genoa kwenye mchezo wa Serie A Jumamosi, aliwaambia waandishi wa habari: "Tunazungumza kuhusu ndoto ya soka, hali ilivyo sasa haiwezi kuihusisha na Inter. Kwa sababu nyingi sana.

"Sidhani kama kuna mtu kichaa duniani ambaye hatamhitaji Messi. Lakini kwa hali jinsi ilivyo, ni mbali, mbali, mbali sana na Inter, kutokana na kile tunachofanya sasa na kile tunachojaribu kukijenga.

"Tunahitaji kujenga msingi imara, na halafu pengine... narudia, hii ni ndoto ya soka; hata hivyo, napenda kusema ukweli kwamba, wakati ndoto ya soka inapokuhusisha, timu inayohusishwa nayo mara zote ni Inter."

Romelu Lukaku alifunga mara mbili kwa kikosi hicho cha Conte na kurudi kwenye kushinda mechi baada ya kupata sare mfululizo.

Alexis Sanchez, ambaye anacheza kwa mkopo kutoka Manchester United aliendelea kuwa kwenye kiwango cha kuvutia na kufunga bao moja, wakati Inter ikijivuta nafasi ya tatu kwenye msimamo, ikiipita pointi moja Atlanta na kupitwa nne na vinara Juventus huku mechi mbili zikiwa zimesalia.

Klabu ya zamani ya Conte, Juventus inaweza kutwaa taji la tisa mfululizo la Ligi Kuu kama jana Jumapili iliifunga Sampdoria.

"Nafikiri kwa sasa tulipo pointi 76, kitu ambacho ni kizuri, lakini nina uhakika hazitoshi kushinda," amesema.

## ZISIKUPITE

### MATUMAINI KWA HAVERTZ

CHELSEA inajiamini kwamba, kiungo wa Bayer Leverkusen mwenye umri wa miaka 21, Kai Havertz, atajiunga na Mjerumani mwenzake, German Timo Werner na kuwa usajili wao wa tatu kipindi hiki cha majira ya joto, hata kama hawatafuzu kwenye ligi ya mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(Mail on Sunday)***

### MESSI AMTAKA BIELSA BARCA

NAHODHA wa Barcelona, Lionel Messi, ameiambia klabu hiyo kwamba kocha wa Leeds United, Marcelo Bielsa anatakiwa achukua mikoba ya Quique Setien na kuwa kocha mpya pale Nou Camp. ***(Sun on Sunday)***

### CRYSTAL YAMUWANIA DYCHE

KLABU ya Crystal Palace inamuwania Sean Dyche wa Burnley kama kocha wao mpya, huku majaliwa ya Roy Hodgson yakiwa shakani baada ya kiwango kibovu msimu huu. ***(Sunday Mirror)***

### SPURS YAMUWANIA WILSON

TOTTENHAM Hotspur inaongoza kwenye mbio za kuwania kumsajili straika wa Bournemouth na England, Callum Wilson, kama timu hiyo itashuka daraja. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 anaweza kupatikana kwa pauni milioni 10. ***(Sun on Sunday)***

### HAKUNA OFA YA KOULIBALY

MKURUGENZI wa Napoli, Cristiano Giuntoli, amesema hakuna ofa yoyote iliyofika mezani kwao kwa ajili ya mlinzi wao wa kati, Kalidou Koulibaly licha ya kuwa na uvumi kwamba nyota huyo wa kimataifa wa Senegal mwenye umri wa miaka 29 anawaniwa na Manchester City, Manchester United, Liverpool na Barcelona. ***(Goal)***

### SOLSKJAER AMWANIA GABRIEL

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, yupo tayari kuingilia usajili wa mlinzi wa kati anayewaniwa na Napoli, Gabriel Magalhaes mwenye umri wa miaka 22 kutoka Lille. ***(Sunday Express)***

### MADDISON AONGEZA MKATABA

KIUNGO wa Leicester, James Maddison , 23, amekataa mpango wa kujiunga Manchester United na amesaini mkataba wa muda mrefu na timu yake hiyo ambapo atakuwa akilipwa pauni 95,000 kwa wiki. ***(Talksport)***

### ARSENAL KUMSAJILI PARTEY

ARSENAL itaweza kusamjili kiungo wa Atletico Madrid, Thomas Partey, pekee kipindi hiki cha majira ya joto, kama wataweza kufikia ada ya pauni milioni 45 iliyopo kwenye mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 raia wa Ghana. ***(Sunday Express)***

### KROOS AHUZUNISHWA NA BALE

KIUNGO wa Real Madrid, Toni Kroos, amesema hali ya mchezaji mwenzake, Gareth Bale klabuni hapo sio nzuri kwa mtu yeyote na nyota huyo mwenye umri wa miaka 31 raia wa Wales alighazabishwa na kuzuiwa kwa uhamisho wake kwenda China kipindi cha majira ya joto kilichopitwa. ***(Goal)***

### SANCHEZ KUSAJILIWA JUMLA

INTER Milan inaangalia uwezekano wa kutaka kumsajili moja kwa moja straika wa Manchester United na Chile, Alexis Sanchez mara baada ya muda wake wa kucheza kwa mkopo hapo kufikia mwisho mwezi ujao. ***(Sky Sports Italia)***

HABARI MICHEZO

## Panama Girls yajipanga kufanya maajabu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Panama Girls umesema wataonyesha maajabu katika michezo yao mitano na timu hiyo kutoshuka daraja, kuendelea kukupigia msimu ujao katika Ligi Kuu ya wanawake Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Katibu Mkuu wa Panama Girls, Satana Chonya, alisema wanashika mkia katika msimamo wa Ligi hiyo ila wana imani ya kufanya vizuri katika mechi hizo tano , mbili wakicheza nyumbani na tatu kucheza ugenini.

Alisema kwa sasa wanaelekea Ruvuma kwenda kutafuta pointi tatu mechi ya ugenini na baada ya hapo wana michezo miwili nyumbani dhidi ya Marshi Queens na Kigoma Sisterz.

"Tutaonyesha maajabu hatushuki daraja, tunapambana kushinda mechi zetu tano kutafuta alama 15 huku tukiwaombea Marsh Queens, Tanzanite na TSC kufanya vibaya katika michezo yao ili tuwe juu katika msimamo," alisema Chonyo.

Alisema wanahitaji kushinda mechi zao zote tano, sababu walikuwepo juu yao wamepishana pointi chache ambazo wanazipata wanaposhinda mechi mbili kwa kupanda na kuwashusha walipo juu.

Chonya alisema wana uhakika wa kufanya vizuri katika mechi zilizobakia na wapo safarini kwenda Ruvuma kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya wenyeji wao Ruvuma Queens.

## Azam kusajili wa kimataifa wenye viwango

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC wameweka mikakati yao ya usajili wa wachezaji wa Kimataifa wenye viwango vizuri ili kurejesha timu hiyo katika ubora kwa ajili ya kuleta ushindani msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara utaotarajiwa kuanza mwanzoni mwa Septemba.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Abdularim Amin 'Popat' alisema wamepanga kufanya usajili kwa maana ya wachezaji wa Kimataifa wenye kiwango cha juu kurejesha ubora wa timu yao.

Alisema usajili huo wataangalia zaidi safu ya ushambuliaji kwa kuleta mchezaji ambaye atakuwa msaada mkubwa katika kikosi kwa msimu ujao wa ligi hiyo.

"Usajili tumemuachia kocha na ameeleza juu ya kufanya usajili wa wachezaji anaowahitaji, ili kuona timu yetu ina rejesha ubora wake hasa msimu ujao kupambana kufanya vizuri na kutwaa ubingwa," alisema Mtendaji huyo.

Alisema msimu ujao utakuwa tofauti na sasa ambayo imemaliza ligi ikiwa nje ya mipango yao na kujipanga kwa msimu ujao inapambana kutwaa ubingwa pamoja na kucheza Michuano ya Kimataifa. Kuhusu kurejea kwa mshambuliaji wao Kipre Tchetche alisema wako katika mpango huo na mambo yakienda vizuri anaweza kurejea ndani ya kikosi cha timu hiyo.

# MKAPA AMEZIBEBA SIMBA SC, YANGA

**Na Somoe Ng'itu,** MOSHI

RAIS Mstaafu wa awamu ya tatu, marehemu Benjamin Mkapa, amezibeba na kuficha aibu ya klabu kongwe nchini za Simba na Yanga kwa kujenga Uwanja wa Taifa ambao ni wa kisasa na unatumika katika michezo yao mbalimbali ya kimataifa, imeelezwa.

**Akizungumza katika mahojiano mubashara juzi usiku, mdau wa michezo, Saleh Ally, alisema uamuzi wa kiongozi huyo kujenga Uwanja wa Taifa umezifanya klabu hizo kunufaika kwa kuutumia kwenye michezo yao ya ndani na ya kimataifa kwa urahisi.**

Ally alisema klabu hizo ambazo hadi leo hazina viwanja vyake binafsi, zinatakiwa kumuenzi kiongozi huyo kwa kufuata nyayo zake kwa kujenga viwanja vyao binafsi hata kama vitaingiza idadi chache ya mashabiki.

"Simba na Yanga wanatakiwa kumuenzi vema Rais Mkapa, amewavisha nguo, amewasitiri aibu yao, Uwanja wa Taifa umekuwa ni uwanja ambao wanautumia kuingiza fedha nyingi katika michezo yao na hivyo unawapa fursa ya kujiimarisha kiuchumi," alisema Ally.

Aliwataka viongozi walioko madarakani wa klabu hizo mbili za jijini Dar es Salaam kuhakikisha wanamuenzi Rais Mkapa kwa kufanya mambo yanayoacha alama ikiwamo kutimiza ndoto za kumiliki viwanja vyao binafsi.

"Hata wakijenga uwanja wenye uwezo wa kuingiza watu 10,000 watakuwa wamefuta aibu ya kutomiliki viwanja, hakika nao watakuwa wameacha kumbukumbu isiyofutika katika klabu zao, wafanye mambo kwa kitendo," alisema mwandishi huyo mwandamizi.

Aliongeza kwa kuwataka wadau wa michezo kujitokeza kwa wingi kumuaga kiongozi huyo kama sehemu ya kumwenzi na itapendeza wakivaa jezi za klabu zao za hapa nchini wanazozishabikia.

"Itapendeza pia kama watavaa jezi za klabu zao kujitambulisha zaidi kama wadau wa soka, waende kumuaga shujaa wetu huku wakijivunia zawadi kubwa aliyotuachia, Simba na Yanga wakicheza kwenye Uwanja wa Taifa wanaingiza zaidi ya milioni 500, ni biashara kubwa sana kwa siku moja " aliongeza.

Marehemu Mkapa anatajwa alikuwa ni mashabiki wa Yanga ingawa aliguswa kujenga Uwanja wa Taifa baada ya kushuhudia umati mkubwa wa mashabiki uliofika kwenye Uwanja wa Ndege kuwapokea Simba waliokuwa wanarejea nchini wakitokea Misri ambapo waliwavua ubingwa wa Afrika, Zamalek mwaka 2003.

Kiongozi huyo aliyefariki nchini usiku wa kuamkia Ijumaa, anatarajiwa kuzikwa kijijini kwao Lupaso, Masasi mkoani Mtwara keshokutwa.




Wachezaji wa timu ya netiboli ya jiji la Tanga, wakifanya mazoezi kujiandaa na mashindano ya Ligi Daraja la Kwanza pamoja na Ligi ya Muungano, itakayofanyika hivi karibuni kwenye Uwanja wa Bandari jijini Tanga. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# *Polisi Tanzania yakataa maproo*

**Na Somoe Ng'itu,** MOSHI

KUELEKEA msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa Polisi Tanzania ya mjini hapa umesema hauna mpango wa kusajili wachezaji wa kigeni katika kikosi chao kinachoshiriki Ligi Kuu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi, amesema usajili wao utaangalia wachezaji wa ndani na wanaamini nyota wenye vipaji wapo hapa nchini.

Munisi alisema watasajili kwa kuzingatia upungufu walioubaini na hawataenda kinyume na mapendekezo yatakayotolewa na benchi la ufundi.

"Hatufikirii wageni, tunaamini wapo wachezaji Watanzania wazuri sana, wakiandaliwa vema wanaweza kushindana na kutupa matokeo mazuri, tuamini vya kwetu, hatufikirii wageni," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kuwa msimu huu ulimalizika jana, kikosi chake kimefanya vema na kinawapongeza wachezaji kwa kujituma katika kila mchezo waliocheza iwe nyumbani au ugenini.

"Kwetu mechi ngumu zilikuwa ni Kanda ya Ziwa, Kyle tuliteseka, pia hatukuwa na ratiba nzuri, kwa mfano Mbeya tumeenda mara mbili, hii ilitusumbua, mwisho wa yote tunamshukuru Mungu tumeonyesha uwezo wetu," Munisi alisema.

Polisi Tanzania na Namungo ya Lindi zilipanda daraja msimu uliopita na kuonyesha ushindani kwenye Ligi Kuu Bara kwa kuzisumbua vigogo wa soka nchini.

Michezo

Jumatatu Julai 27, 2020

Nipashe



Conte afurahishwa Messi kutajwa Inter

UKURASA 22



Wachezaji na baadhi ya viongozi wa Simba, wakisherehekea ubingwa kwenye uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini Mtwara, baada ya kukamilika mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Ndanda na kutwaa ubingwa msimu wa 2019/20, ikiwa pia ni kwa mara ya tatu mfululizo. **PICHA: MAKTABA**

# 19-20 msimu wa tabu

## Yanga yaishusha Lipuli, huku Ndanda, Alliance nazo zikishuka, Mbao, Mbeya City kucheza mchujo...

**Isaac Kijoti,** IRINGA **na Somoe Ng'itu,** MOSHI

MSIMU wa Ligi Kuu Bara 2019-20, umekuwa wa tabu kuanzia kwa wenye mpira wao, Shirikisho la Soka nchini (TFF) hadi klabu shiriki katika ligi hiyo iliyoshirikisha timu 20.

**Ligi hiyo msimu huu imekuwa ngumu kutokana na kulazimika kusimama kwa takriban miezi mitatu kuanzia Machi 17 hadi iliporejea tena Juni 13, mwaka huu.**

Kusimama kwa ligi hiyo kulitokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19, hatua ambayo iliifanya TFF kuwa katika wakati mgumu wa kuamua bingwa na timu zitakazoshuka daraja.

Hata hivyo, juhudi za serikali katika kupambana na ugonjwa huo zilizaa matunda, hivyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Magufuli kuruhusu Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili kurejea.

Ligi hiyo ambayo ilisimama zikiwa zimebaki raundi 10 kumalizika, imemalizika jana Simba ikiwa imehitimisha shughuli za ubingwa mapema na vita kubwa ilibaki kwa timu za kushuka daraja moja kwa moja za kucheza mechi za mchujo na kusaka nafasi ya pili.

Na jana vita hivyo vimemalizika kwa Yanga kumaliza nafasi ya pili baada ya kutoka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Lipuli FC katika Uwanja wa Samora huku Azam FC iliyokuwa ikicheza dhidi ya Tanzania Prisons katika Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya ikilala kwa mabao 2-1 na kumaliza nafasi ya tatu kwa pointi 69, tatu nyuma ya Yanga.

Bao la Yanga katika mechi hiyo iliyokuwa kali na ya kusisimua Lipuli ikihitaji ushindi ili kubaki Ligi Kuu msimu ujao ilijikuta ikizamishwa na David Molinga dakika ya 39 akiitendea haki pasi ya Mrisho Ngasa.

Baada ya ushindi huo, mashabiki na wachezaji wa Yanga walishangilia kama mabingwa huku Kocha Luc Eymael akisindikizwa kutoka uwanjani kutokana na kila mmoja kutaka kumpongeza.

Mabingwa Simba wakiwa katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi dhidi ya Polisi Tanzania, walihitimisha ligi hiyo kwa ushindi wa mabao 2-1 yakifungwa na nahodha John Bocco dakika ya pili na 44 huku lile la wenyeji likifungwa na Marcelo Kaheza kwa mkwaju wa penalti dakika ya 32.

Kwa upande wa Azam FC ikiwa Uwanja wa Samora jijini Mbeya dhidi ya wenyeji Tanzania Prisons iliambulia sare ya mabao 2-2, hivyo kumaliza katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 70 mbili nyuma ya Yanga.

Kwingineko kulikuwa na tabu nyingine katika viwanja sita ambapo vita kali ilikuwa nani ashuke daraja na yupi wa kucheza mechi za mchujo ili kupata timu mbili kuungana na zingine 16 zitakazoshiriki Ligi Kuu msimu ujao. Ndanda FC imeshuka daraja baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya Mbao FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza, hivyo kubakia na pointi zake 41, ikishika nafasi ya 19 ambayo ni ya mwisho kutoka mkiani.

Alliance FC, pamoja na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Namungo kwenye Uwanja wa Nyamagana mjini Mwanza, bado haukuiwezesha kubaki Ligi Kuu, nayo imeshuka moja kwa moja, ikimaliza na pointi 45, lakini ikiwa kwenye nafasi ya 17.

Kilichoiponza Alliance ni uwiano mdogo wa magoli ya kufunga na kufungwa, tofauti na timu za Mbao FC na Mbeya City ambazo zitacheza mechi za mchujo na timu za Ihefu na Geita Gold.

Mbao FC, ikiwa CCM Kirumba imeadhibu Ndanda mabao 2-0 na kuifanya kufikisha pointi 45, ikishika nafasi ya 16 ambayo imeifanya kwenda kucheza mechi ya mchujo kujua majaliwa yake.

Mbeya City imeachia kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya KMC, na kuifanya nayo kufikisha pointi 45, ikiwa kwenye nafasi ya 15, nayo pia inakwenda kwenye mechi ya mchujo.

Bahati iliiangukia Mtibwa Sugar kuepuka kushuka daraja, kwani pamoja nayo kuwa na piointi 45, ikiichapa Ruvu Shooting mabao 2-1, lakini uwiano mzuri wa mabao ya kufunga na kufungwa umeiokoa.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042